



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TEHAMA NI MSINGI WA TAIFA ENDELEVU;  
ITUMIE KWA USAHIHI NA UWAJIBIKAJI**

**"Kupambana na  
Rushwa ni Jukumu  
langu "**

**"Mshikamano wa  
Kitaifa tuwajibike kwa  
pamoja"**



**2021**

**"Tujenge jamii yenye  
Afya Imara kwa  
kuzingatia Lishe bora"**

**"Ziro malaria Inaanza  
na Mimi- Chukua  
hatua kuitokomeza"**

**Elimu sahihi juu ya Dawa za Kulevya Huboresha Huduma kwa Waraibu: Chukua hatua**



NUKUU YA BABA WA TAIFA KUHUSU MWENGE WA UHURU.....	1.
NUKUU YA RAIS WA JUMUHURI YA TANZANIA KUHUSU TEHAMA.....	2
RAMANI YA WILAYA YA NEWALA .....	3
RATIBA YA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU 2021.....	4-6
SALAMAU ZA MHE. MKUU WA WILAYA .....	7-9
GHARAMA ZA MIRADI YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021 .....	10
TAARIFA YA MRADI WA VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI MAKUKWE...	11
TAARIFA YA KLABU YA WAPINGA RUSHWA.....	13
TAARIFA YA VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI .....	14
TAARIFA FUPI YA MRADI WA BARABARA YA KIDUNI.....	16
TAARIFA YA FUPI YA MRADI WA MAJI CHITANDI.....	18
TAARIFA YA FUPI YA UJENZI WA KIWANDA CHA NAFKA CHA HKM SUPER SEMBE...	20
TAARIFA YA FUPI YA ZAHANATI YA TUPENDANE .....	22
TAARIFA YA MIFUMO YA TEHAMA KATIKA ZAHANATI.....	24-25
TAARIFA YA FUPI YA LISHE.....	27- 28
TAARIFA FUPI YA TEHAMA KATIKA BANDA.....	30
TAARIFA FUPI YA SHUGHULI ZA MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI.....	32
TAARIFA FUPI YA SHUGHULI ZA MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA .....	33
TAARIFA FUPI MAPAMBANO DHIDI YA MADAWA YA KULEVYA.....	35-36
TAARIFA YA BANDA LA TAKUKURU (W).....	37-38
TAARIFA NA TAKWIMU MYHIMU KUHUSU WATU WENYE ULEMAVU.....	39
RISALA YA WANANCHI YA UTII KWA RAIS.....	41-48
VIAMBATISHO .....	49-64
SALAMU ZA MKUU WA WILAYA KWENYE MAKABIDHIANO.....	65 - 66
ORODHA YA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2019.....	67

## ORODHA YA PICHA NA VIELELEZO

<b>PICHA / KIELELEZO</b>	<b>UKURASA</b>
Kielelezo 1: SHELE YA SEKONDARI MAKUKWE.....	14
Kielelezo 2: BODABODA WAKIKABIDHIWA PIKIPIKI .....	16
Kielelezo 3: PICHA YA BARABARA YA KIDUNI .....	18
Kielelezo 4: PICHA YA MRADI WA CHITANDI .....	20
Kielelezo 5: PICHA YA KIWANDA CHA NAFKA .....	23
Kielelezo 6: PICHA ZA ZAHANATI YA TUPENDANE. ....	41
Kielelezo 7: PICHA YA MTAALAMU WA AFYA AKITOA HUDUMA KWA NJIA YA AFYA ....	42
Kielelezo 8: PICHA KUHUSU LISHE.....	14
Kielelezo 9: PICHA ZA KUHUSU TEHAMA .....	16
Kielelezo 10: PICHA ZA KUHUSU KUDHIBITI MALARIA .....	18
Kielelezo 11: VIAMBATISHO A - H.....	49-64

# NUKUU YA BABA WA TAIFA KUHUSU MWENGE



## BABA WA TAIFA

### MWALIMU JULIUS KAMBARAGE NYERERE


*"Falsafa ya Mwalimu Julias Kambarage Nyerere kuhusu mwenge wa uhuru, wakati akitoa hotuba ya siku ya Uhuru tarehe 9/12/1961; aliwatangazia wataanzania, Afrika na Dunia kwa ujumla kwa kuyarudia maneno hayo kwa kusema "Sisi tumekwisha uwasha mwenge wa uhuru na kuuweka juu ya mlima Kilimanjaro, umulike ndani na nje ya mipaka yetu, ulete matumaini pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima palipo jaa dharau.*

**NUKUU YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE  
SAMIA SULUHU HASSAN**



***“Dunia ipo kwenye Mapinduzi ya Nne ya Viwanda, ambayo yanaongozwa na sekta ya Teknolojia ya Mawasiliano (TEHAMA), na kwa maana hiyo, Uchumi wa dunia pamoja na shughuli nyingi duniani, kwa sasa, zinafanyika kwa kutumia TEHAMA. ....”*** Aliyasema hayo Wakati wa kulihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dodoma, Aprili 2021.

# Newala District: Divisions, Wards and Villages and Road Network



**RATIBA YA MPIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021**  
**WILAYA NEWALA**

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI Km	TUKIO/SHUGHULI	WAHUSIKA
30/08/2021	12:00 - 2:00	Makukwe	0	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya Tandahimba (eneo la Shule ya msingi Makukwe II)</li> </ul>	DC na wananchi
	2:00 - 2:10	Makukwe	5	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Nnauja ndani ya gari kuelekea Makukwe sekondari</li> </ul>	DC
	2:10 - 3:10	Makukwe Sekondari		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Mradi Madarasa</li> <li>• Kufungua Madarasa 2 na Ofisi 1 shule ya Sekondari Makukwe</li> <li>• Taarifa ya klabu ya Rushwa</li> <li>• Kuzindua Klabu ya Kupinga Rushwa Shuleni hapo.</li> </ul>	DC na wananchi
	3:10-3:25	Makukwe sekondari	12	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Mtunguru ndani ya gari kuelekea Ushirika sekondari</li> </ul>	DC
	3:25 - 4:55	Ushirika sekondari		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Mradi</li> <li>• Kugawa pikipiki 15 kwa vikundi 2 vya Bodaboda na Bajaji 1 kwa kikundi 1 cha walemavu pamoja na kuona/kukagua shughuli za vikundi vya wajasiliamali, wanawake na wenye Ulemavu eneo la Shule ya Sekondari Ushirika.</li> <li>• <b>UJUMBE WA MWENGE</b></li> <li>• <b>CHAI</b></li> </ul>	DC na wananchi
	4:55 - 5:15	Ushirika sekondari	21	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Magombo, Londo Namiyonga, mahumbika ndani ya Gari kuelekea Kiduni</li> </ul>	DC
	5:15-6:15	Kiduni		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Mradi</li> <li>• Kuweka jiwe la Msingi ujenzi wa Barabara ya Kiduni - Makondeko <b>KM 1</b> ya kiwango cha Lami.</li> </ul>	DC na Wananchi
	6:15 - 6:25	Kiduni	8	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Julia</li> </ul>	DC

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI Km	TUKIO/SHUGHULI	WAHUSIKA
				ndani ya Gari kuelekea Nangwala Juu	
	6:25 - 7:20	Nangwala Juu		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Mradi</li> <li>• Kuona/kukagua ujenzi wa Mradi wa Maji Chitandi</li> </ul>	DC na wananchi
	7:20-7:25	Nangwala Juu	3	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kuelekea Newala day</li> </ul>	DC
	7:25 - 8:10	Newala Day		<ul style="list-style-type: none"> <li>• <b>BURUDANI</b></li> <li>• <b>UJUMBE WA MWENGE</b></li> <li>• <b>CHAKULA CHA MCHANA</b></li> </ul>	DC na wananchi
	8:10 - 8:20	Newala Day	8	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Amkeni ndani ya gari kuelekea Tulindane</li> </ul>	DC
	8:20 - 9:20	Tulindane		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Mradi</li> <li>• Kuzindua Kiwanda cha Kusaga na Kukoboa Nafaka cha Kampuni ya HKM</li> </ul>	DC na wananchi
	9:20-9:23	Tulindane	1	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kuelekea Tupendane</li> </ul>	DC
	9:23-10:23	Tupendane		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Utambulisho</li> <li>• Taarifa ya Zahanati</li> <li>• Kuona/kukagua na kupata taarifa ya Mifumo ya <b>TEHAMA</b></li> <li>• Kuzindua Zahanati ya Tupendane</li> <li>• Kupata taarifa ya wilaya ya Lishe na kukagua banda la kutoa Elimu ya Lishe.</li> </ul>	DC na wananchi
	10:23-10:30	Tupendane	7	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Amkeni ndani ya gari kuelekea Luchingu (stand)</li> </ul>	DC
	10:30 -	Luchingu (stand)		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kuona na kukagua juhudi za Wilaya katika kutoa <b>ELIMU YA TEHAMA, LISHE</b>, kupambana na <b>MALARIA, UKIMWI, MADAWA YA KULEVYA NA RUSHWA.</b></li> <li>• <b>RISALA YA UTII</b></li> <li>• <b>UJUMBE WA MWENGE</b></li> <li>• <b>BURUDANI</b></li> <li>• <b>CHAKULA CHA JIONI</b></li> </ul>	DC na wananchi

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI Km	TUKIO/SHUGHULI	WAHUSIKA
				<ul style="list-style-type: none"> <li>• MKESHA</li> </ul>	
31/08/2021	12:00-1:00	Luchingu (Stand)	0	<ul style="list-style-type: none"> <li>• CHAI</li> <li>• Kupata taarifa ya vipimo vya HIV/Ukimwi</li> </ul>	DC na wananchi
	1:00 -1:20	Luchingu (stand)	16	<ul style="list-style-type: none"> <li>• Mwenge wa Uhuru kupita Amkeni, Nambunga ndani ya gari kuelekea Mitesa</li> </ul>	DC
	1:20	Mitesa		<ul style="list-style-type: none"> <li>• Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Wilaya ya Masasi</li> </ul>	DC na wananchi
	<b>JUMLA</b>		<b>81</b>		

**SALAMU ZA MHE. MKUU WA WILAYA KWENYE  
MAPOKEZI YA MWENGE WA UHURU TAREHE 30/08/2021**

Ndugu, Luteni Josephine Paul, Kiongozi wa Mbio Maalum za mwenge Kitaifa 2021

Ndugu, Wakimbiza Mwenge wote Kitaifa

Ndugu, Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama (W)

Ndugu, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Newala

Ndugu. Katibu wa CCM Wilaya ya Newala

Wahe, Wabunge wa Majimbo ya Newala Mji na Newala vijijini

Wah, Madiwani

Wah, Viongozi Vyama vya Siasa

Ndugu, Viongozi wa Dini, Wakuu wa Taasisi na Mashirika na binafsi, Watendaji wa

Serikali, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Wanahabari, Wananchi wote wa

Newala mliondhorua Mabibi na Mabwana

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kibali cha kufanya zoezi hili muhimu la kupokea na kukimbiza mwenge wa uhuru katika wilaya yetu ya Newala. Napenda kuwapongeza sana wakimbiza Mwenge wa kitaifa na wakufunzi wao kwa kuukimbiza Mwenge wa uhuru salama na kueneza ujumbe wa Mwenge kwa wananchi wenzetu kote mwenge huu ulikopita.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Mwenge wa Uhuru ukiwa Wilaya ya Newala utakimbizwa umbali wa km **81**, tarafa **2** kata **10** na vijiji **23**. Aidha, Mwenge wa Uhuru utatembelea miradi **7** ya sekta za Elimu, Afya Miundombinu, maji, Viwanda, Maendeleo ya Jamii na utekelezaji wa ujumbe wa mwenge wa Uhuru. Kati ya hiyo mradi **1** utawekewa mawe ya msingi, miradi **3** itazinduliwa, **1** utafunguliwa, miradi **2** itaonwa na kukaguliwa (vijana na ujumbe wa mwenge) kwa mchanganuo ufuatavyo;

**Miradi itakayo tembelewa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2021.**

S/N	SEKTA	KUFUNGUA	KUZINDUA	JIWE LA MSINGI	KUONA/KUKAGUA	JUMLA
1	Elimu	1				1
2	Afya		1			1
3	Viwanda		1			1
4	Vijana na Akina mama				1	1
5	Maji				1	1
6	Mawasiliano/Barabara			1		1
7	Utawala bora,		1			1
	<b>JUMLA</b>	<b>1</b>	<b>3</b>	<b>1</b>	<b>2</b>	<b>7</b>

Miradi hii imezingatia ujumbe wa mwenge wa mwaka 2021 kwa ujumla Miradi yote **7** ina jumla ya thamani ya shilingi **1,722,812,765.74/-** kwa mchanganuo ufuatao

<b>MCHANGO</b>	<b>THAMANI</b>	<b>ASILIMIA YA MCHANGO</b>
Wananchi	113,007,000.00	6.56
Wilaya	48,000,000.00	2.79
Serikali Kuu	1,404,451,502.35	81.52
Wahisani	157,354,263.39	9.13
<b>Jumla</b>	<b>1,722,812,765.74</b>	<b>100</b>

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Mwenge wa Uhuru mwaka 2021, umebeba ujumbe wa TEHAMA usemao **“TEHAMA ni msingi wa Taifa endelevu; itumie kwa usahihi na uwajibikaji”**. Wilaya inatambua jitihada zinazofanywa na serikali ya awamu ya sita katika kusimamia matumizi sahihi ya mfumo wa TEHAMA, Lishe bora kupambana na magonjwa ya kuambukiza VVU/UKIMWI na U-Viko (COVID-19).

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wananchi wa Wilaya ya Newala tuko katika mapambano dhidi ya maadui wa maendeleo ambao ni Umasikini, Ujinga, Maradhi na mapambano dhidi ya **RUSHWA, UKIMWI, DAWA ZA KULEVYA**, na **MALARIA**. Aidha Wilaya inaendelea kuelimisha jamii kupitia Radio Newala na mikutano ya hadhara.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Shughuli za uzalishaji mali kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu vinaendelea kupewa kipaumbele ambapo Wilaya inawezesha vikundi kupata mikopo yenye masharti nafuu kila mwaka. Lengo la kuviwezesha vikundi hivi ni kuwaongezea kipato, kuwaepusha na makundi yasiyofaa kama kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya, biashara haramu ya usafirishaji wa madawa ya kulevya, kujiuza miili, kushiriki ngono zembe zinazoweza kuhatarisha afya zao na kuwaletea maambukizi ya UKIMWI hivyo kupunguza nguvu kazi ya taifa.

## **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wananchi wa Newala wana hamu kubwa sana ya kuuona Mwenge wa Uhuru na kuusikia Ujumbe wa Mwenge, hivyo niwashukuru wote kwa kunisikiliza na nitamke sasa kwa heshima na taadhima tuko tayari kuanza mbio maalum za Mwenge wa Uhuru Mwaka 2021. Ahadi yangu kwenu ni ulinzi na usalama wa Mwenge na Msafara wote kwa ujumla.

**Mungu Ibariki Afrika**

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Kazi iendelee**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

.....  
**MHE. MWANGI RAJAB. KUNDYA**

**MKUU WA WILAYA**

**NEWALA**

**30/08/2021**

**GHARAMA ZA MIRADI YA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2021 WILAYA YA NEWALA**

NA	SEKTA		MRADI	TUKIO	MCHANGANUO WA GHARAMA TSHS				
					WANANCHI	WILAYA	S/KUU	WAHISANI	JUMLA
1	Afya	1	Ujenzi wa zahanati ya Mtaa wa Tupendane	Kuzindua zahanati	-	-	-	117,354,263.39	117,354,263.39
2	Maji	2	Ujenzi wa miundombinu ya maji- Chitandi	Kuona/kukagua		-	927,392,502		927,392,502
3	Miundombinu	3	Ujenzi wa barabara ya Kiduni-Makondeko kwa kiwango cha lami KM 1	Kuweka jiwe la Msingi barabara KM 1 ya lami	-	-	477,500,094	-	477,500,094
4	kilimo	4	Kampuni ya HKM Super Sembe	Kuzindua	111,007,000	-	-		111,007,000
5	Elimu	5	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Shule ya Sekondari Makukwe	Kufungua vyumba vya madarasa	2,000,000	4,000,000	-	40,000,000	46,000,000
6	Maendeleo ya Jamii	7	Kikundi cha Pikipiki Kitangali	Kukabidhi pikipiki kwa Vijana		44,000,000	-		44,000,000
7	Miradi ya ujumbe wa mwenge	8	Kuona na kupata taarifa ya wilaya katika juhudi ya Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rushwa, Malaria, UKIMWI na Lishe bora za mitaa	kukagua na kuona shughuli za mapambano dhidi ya Rushwa, UKIMWI, Malaria, Madawa ya kulevya na Lishe bora	-	-	-	-	-
	<b>JUMLA KUU</b>				<b>113,007,000</b>	<b>48,000,000</b>	<b>1,404,451,502.35</b>	<b>157,354,263.39</b>	<b>1,722,812,765.74</b>

**TAARIFA FUPI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA SHULE YA SEKONDARI  
MAKUKWE KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA  
KWA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Shule ya sekondari Makukwe ina jumla ya wanafunzi 630 kati yao wavulana ni 266 na wasichana ni 364 Shule ina mahitaji ya vyumba vya madarasa 16 na matundu ya vyoo 30. Shule natumia mifumo ya **TEHAMA** ambayo ni **PREMS, SIS, BEMIS** na **FFARS** kwa ajili ya kuwapunguzia wazazi na wazabuni bughuza wakati wa usajili, uhamisho wa wanafunzi na malipo ya wazabuni.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Shule ina mradi wa ujenzi wa vyumba **2** vya madarasa na ofisi 1. Mradi huu umeanza kutekelezwa mwezi Mei 2021. Mradi una thamani ya Tshs **46,000,000/=** ambapo Tshs **40,000,000** ni fedha za Wahisani, Tshs **4,000,000** ni fedha za wilaya na Tshs **2,000,000/=** ni nguvu za wananchi.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Mradi umekamilika kwa **100%** na umetumia jumla ya Tshs **46,000,000** kwa shughuli za ununuzi wa vifaa vya ujenzi, ufundi na utengenezaji wa viti **80** na meza **80** Kukamilika kwa mradi huu kumewezesha kupunguza msongamano wa wanafunzi kwa darasa.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague na utufungulie vyumba vya madarasa na ofisi.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyeeee!!!**

## PICHA YA VYUMBA VYA MADARASA 2 NA OFISI SHULE YA SEKONDARI



**TAARIFA FUPI YA UZINDUZI WA KLABU YA WAPINGA RUSHWA SHULE YA  
SEKONDARI MAKUKWE KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA  
UHURU KITAIFA KWA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Klabu ya Wapinga Rushwa katika Shule ya sekondari ya MAKUKWE ni moja kati ya vilabu vya Wapinga Rushwa 26 vilivyoanzishwa katika shule za Sekondari Wilayani Newala.

Klabu ya wapinga Rushwa Shule ya sekondari MAKUKWE ina jumla ya Wanachama **81** ikiwa wavulana **22** na wasichana **59**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Vilabu vya wapinga Rushwa katika Shule za sekondari vimeanzishwa kwa lengo la kuwajenga wanafunzi kimaadili na kuwashirikisha katika Mapambano dhidi ya Rushwa kwa:-

- Kuwezesha vijana kutambua nafasi na wajibu wao katika Mapambano dhidi ya Rushwa na hivyo kushiriki ipasavyo katika Kuzuia na Kupambana na Rushwa.
- Kuwajenga vijana kimaadili kwa kuwafanya watambue madhara ya Rushwa ili waichukie katika maisha yao na hatimaye kujenga jamii ya watu waadilifu.
- Kuiwezesha jamii nzima kutambua nafasi na wajibu wao katika Mapambano dhidi ya Rushwa.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Jukumu la Kupambana na Rushwa si la TAKUKURU wala Serikali peke yake bali ni la kila raia. Hivyo ni wajibu wetu sote kushiriki kikamilifu katika Mapambano haya kwani kwa pamoja tutashinda. Kama Ujumbe wa mwenge mwaka 2021 katika kauli inavyosema **"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"**. Hivyo sisi Wanachama wa klabu ya wapinga Rushwa Shule ya sekondari MAKUKWE tunashirikiana na TAKUKURU katika kutoa elimu kwa jamii yetu ili waweze kushiriki katika mapambano dhidi ya Rushwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba utuzindulie rasmi klabu yetu ya wapinga Rushwa shule ya sekondari MAKUKWE.

**ASANTE, KARIBU NEWALA**

**Mwenge Oyeeeeeee!**

**TAARIFA FUPI YA MIRADI YA VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI PAMOJA NA KUKABIDHI  
PIKIPIKI 15 KWA VIJANA WA BODABODA NA BAJAJI 1 KWA KIKUNDI CHA  
WALEMAVU KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA  
LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI, TAREHE 30/08/2021.**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru,**

Wilaya ya Newala imeendelea kutenga asilimia **10%** ya mapato yake ya ndani na kuwezesha vikundi vya kiuchumi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili kupambana na adui umasikini. Lengo kuu ikiwa ni kuvijengea uwezo vikundi, kuongeza kipato, kuwasaidia katika kufikia fursa mbalimbali na kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru,**

Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Wilaya imetenga asilimia **10%** Tshs **197,905,962/=** ya mapato halisi ya Tsh. **1,979,059,616/=**. Aidha, Wilaya imetoa mikopo kupitia fedha za marejesho kiasi cha Tshs. **179,671,591/-**. Hadi kufikia Juni 2021, Wilaya imetoa mikopo kwa wanufaika **714** katika vikundi **78** (vijana **27**, wanawake **43** na walemavu **7**). Katika bajeti ya mwaka 2021/2022 Wilaya imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya Tsh **234,166,200/=** kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru,**

Vikundi vya vijana na wanawake walionufaika na mikopo hii wanafanya shughuli za viwanda vidogo vidogo visivyohitaji mitaji mikubwa. Shughuli hizo zinajikita katika sekta za kilimo na ufugaji, usindikaji wa mazao kama vile mihogo, mahindi na korosho, uchomeleaji vyuma, useremala, ushonaji, uchoraji na upakaji rangi majengo, utengenezaji wa sabuni za maji, batiki, ususi, biashara ndogo ndogo, bodaboda, utengenezaji vikapu na viatu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru,**

Kwa kujiunga katika vikundi hasa kwa vijana pamekuwa na faida mbalimbali hususani kuondoa utegemezi na kujitengenezea ajira, kupata elimu ya ujasiriamali, na kuepusha vijana wengi kujiunga na vikundi visivyofaa kama uvutaji bangi na madawa ya kulevya.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru,**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague na kuona baadhi ya shughuli za vikundi vya wajasiriamali pamoja na kukabidhi Pikipiki **15** kwa vijana wa Bodaboda na Bajaji 1 kwa kikundi cha watu wenye ulemavu.

**ASANTE, KARIBU NEWALA**

**Mwenge wa Uhuru Oyeeee**

**VIJANA WA KIKABIDHIWA BODABODA NA. MKUU WA WILAYA**



**MKUU WA WILAYA AKIKABIDHI PIKIPIKI**



**KIJANA WA BODABODA AKIONYESHA KADI YA PIKIPIKI BAADA WA KUKABIDHIWA NA MKUU WA WILAYA**

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA BARABARA YA KIDUNI KWA KIONGOZI WA MBIO  
MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI  
TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Barabara ya Kiduni ina urefu wa Km 1 na inasimamiwa na wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA). Barabara hii inafanyiwa matengenezo ya kiwango cha lami ili kuimarisha huduma za Barabara kwa wananchi zaidi ya 12,015 wa maeneo ya karibu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Matengenezo ya barabara hii yanafanywa na Mkandarasi Mzawa **Makapo Contractors & General Supplies Co. LTD** na yanagharimu jumla ya Tshs. **477,059,000/=** ikijumuisha utengenezaji wa barabara, makaravati na mifereji ya mawe. Matengenezo yalianza tarehe 01/12/2020 na yanatarajiwa kukamilika tarehe 30/08/2021 kwa mujibu wa mkataba.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Matengenezo haya yana lengo la kutatua tatizo la uharibifu wa barabara wa mara kwa mara hasa wakati wa mvua, Kutatua changamoto ya usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwa wananchi wa Newala . Pia, kutatua changamoto ya mmomonyoko wa udongo kwa mujibu wa aina ya udongo na jiografia wa Newala ambayo iko mita 800 kutoka usawa wa bahari. Aidha, barabara hii ni ya ulinzi kuelekea mpaka wa Tanzania na Msumbiji.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague na utuwekee jiwe la msingi mradi wetu wa Barabara ya Kiduni - Makondeko.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**PICHA ZA UJENIZ WA BARABARA YA KIDUNI MAKONDEKO KWA KIWANGO CHA LAMI**



**UJENZI WA BARABARA YA KIDUNI MAKONDEKO UKIWA KATIKA HATUA YA AWALI**



**SAMPULI YA UDONGO IKICHUKULIWA KWA AJILI YA KUPELEKWA MAABARA**



**UTEKELEZAJI WA BARABARA YA KIDUNI-MAKONDEKO UNAENDELEA**

**TAARIFA FUPI YA MRADI WA WA MAJI CHITANDI KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM  
ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE  
30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Mradi wa maji Chitandi ni mradi wa uboreshaji wa huduma ya Maji katika mji wa Newala, mradi huu umeanza kutekelezwa mnamo mwaka 2018 na unatekelezwa na kampuni ya ujenzi ya **SINGILIMO ENTERPRISES LIMITED** yenye makao makuu jijini Dar es Salaamu. Mradi unatarajiwa kukamilika mnamo mwezi December 2021 na kwa sasa mradi umefikia **75%** ya utekelezaji, ambapo mradi huu unahusisha vijiji/mitaa ambayo ni Chitandi, Luchingu-Amkeni, na Nangwala (Machinjioni) kwa lengo la kuboresha huduma ya maji safi na Salama Mjini Newala.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Jumla ya **Tshs 927,392,502.35** zitatumika katika utekelezaji wa Mradi, kwa Ujenzi wa tenki la lita **500,000**, Mtandao wa Bomba, Ujenzi wa matenki matatu lita **25,000** katika mwinuko wa mita **3**, Ujenzi wa vituo vya kuchotea Maji **5** na vioski **2**.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Hadi mwezi Julai 2021, Jumla ya **Tshs. 396,747,565.12** sawa na asilimia **43** zimetumika katika utekelezaji wa Mradi ambao hatua ya Ujenzi wa Matenki **3** ya **25m<sup>3</sup>** mnara wa mita **3** juu uliofikia **90%**, Ulazaji wa Bomba **9.907** km uliofikia **98%** na Ujenzi wa vituo **5** vya kutolea Maji umekamilika na vinatumika. Ujenzi wa Tenki lita **500,000** uliofikia **30%**. Kukamilika kwa Mradi huu, Jumla ya wakazi wapatao **15,328** watapata huduma ya Maji safi na salama ambapo (Chitandi **1,523**), Luchingu-Amkeni **6,918**, Nangwala -Machinjioni **6,887**.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Mradi huu umechelewa kukamilika kutokana na Fedha za mradi kuchelewa kutolewa. Aidha, Serikali imeendela kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukagwe na uone mradi wetu wa maji – Chitandi.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**PICHA ZA MARADI WA MAJI CHITANDI**



**UJEZNI WA TANKI LA LITA 500,000**



**TANKI LA JUU LA MAJI**



**KITUO CHA KUTOLEA MAJI**

**TAARIFA FUPI YA UJENZI WA KIWANDA CHA NAFKA CHA HKM SUPER SEMBE KWA  
KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE  
PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kiwanda cha HKM super Sembe ni kiwanda cha sekta binafsi ambacho kilianza ujenzi mwaka 2020. Kiwanda kina milikiwa kwa ubia na wajasiriamali Ndugu. Mohamed Selemani Mohamed na Ndugu. Asiimwe Eladia Batamuzi.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kiwanda hiki kimegharimu kiasi cha Tsh: **111,007,000/=** ambapo Tshs. **92,467,000/-** ni gharama za jengo la mashine, mgahawa, Ghala/stoo ya kuhifadhia unga na nafaka, ofisi, uzio, majengo ya huduma za kijamii na Tshs. **18,540,000/-** ni gharama ya mitambo/mashine. Aidha, kiwanda kinaendelea na ukamilishaji wa jengo la kukamulia mafuta ya alizeti. Kiwanda kimepata fedha kutokana na shughuli za ujasiriamali na Mkopo kutoka benki.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kiwanda kina lengo la kuchakata unga Tani 60 kwa mwaka na kimetoa ajira 7 sawa na 44 % ya lengo la kutoa ajira 16 rasmi na zisizo rasmi. Aidha, kiwanda kinatarajia kunufaisha jamii yote ya ndani na nje ya Newala kwa kununua Malighafi na kuuza bidha (Unga safi na salama, mafuta ya alizeti, pumba na mashudu).

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba ukague na uzindue mradi wa Kiwanda cha HKM Super Sembe.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**Ndugu. Mohamed Selemani Mohamed.  
Mkurugenzi wa Kiwanda  
HKM Super Sembe.**

# PICHA YA KIWANDA CHA NAFKA CHA HKM SUPER SEMBE



**TAARIFA FUPI YA ZAHANATI YA TUPENDANE KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA  
MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE**

**30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Zahanati ya Tupendane iko kata ya Tulindane yenye wakazi zaidi watu **5,413** . Zahanati hii ilianza kujengwa mwaka 2018 na ilikaguliwa na kuwekewa jive la msingi na kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru wa mwaka 2019 ulioambatana na upandaji miti kwa ajili ya utunzaji mazingira. Kituo kimekamiliwa, kimesajiliwa kwa namba **1136159** mwaka **21/09/2019** na kilianza kutoa huduma mwaka **2020**. Kituo kinatumia mfumo wa Mfumo wa TEHAMA ( **GoT-Homis** )

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Zahanati ya Tupendane imejengwa kwa fedha za TASAF kiasi cha Tsh. **117,354,263.39** kati ya fedha hizi Tsh. **89,023,000/=** Zilitumika kujenga jengo la kutolea huduma OPD lenye vyumba **13**, Matundu ya vyoo **8**, Kichomea taka za zahanati na Shimo la kutupia Kondo la Nyuma (Placenta pit), kiasi cha Tsh. **11,236,263.39/=** zilitumika kuibua, kujengea uwezo kamati ya mradi CMC na usimamizi wa mradi, na Tsh. **17,095,000/=** zilitumika kununulia samani za zahanati na vifaa tiba.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Katika kuhakikisha utoaji wa huduma bora na usimamiaji wa mapato ya zahanati, Wilaya imefunga Mfumo wa TEHAMA wa GoT-Homis ambao unarahisisha utoaji wa huduma mbali mbali kama Bima za Afya, Utunzaji wa kumbukumbu za wateja, dawa na vifaa tiba.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Kukamilika kwa zahanati hii kumewezesha wananchi wa kata ya Tulindane kunufaika na huduma za matibabu, kliniki ya mama, baba na mtoto (RCH), huduma za chanjo na uzazi. Tangu kituo kianza, kimeweza kutoa huduma kwa wagonjwa **2,643** wa nje (OPD), huduma ya uzazi kwa kinamama **92**, huduma ya kliniki ya kinamama wajawazito **165**, huduma ya kliniki kwa watoto **3,436** chini ya miaka 5 imetolewa, Huduma ya chanjo imetolewa kwa watoto **2,449**. Kwa ujumla zahanati hii imesaidia kupunguza msongamano katika Hospitali ya wilaya Newala.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba uzindue zahanati ya Tupendane.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**Sophia Makungu  
Afisa Mipango**

## PICHA YA ZAHANATI YA TUPENDANE



**TAARIFA FUPI YA MIFUMO YA TEHAMA KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA  
MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE  
30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Maboresho yanayoendelea kufanyika katika sekta ya mawasilino na Afya yanaboresha huduma na kuongeza ufanisi kwa watumishi wa umma katika kuhudumia jamii. Wilaya ya Newala imejiwekea mpango wa kuhakikisha huduma zote zinazotolewa katika vituo vya kutolea huduma inapatikana kwa kupitia mifumo ya TEHAMA ili kuongeza tija , ufanisi na kuokoa upotevu wa fedha .

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Mfumo wa utoaji wa utoaji huduma wa GoTHomis umewekwa katika Vituo vya kutolea huduma za afya **13** kati ya **42** ,katika zahanati hii mfumo unatumika katika dirisha la usajili/malipo, daktari, maabara na dirisha la kutoa dawa/bohari ya dawa.mfumo huu unawezesha huduma zote za kiasia kutolewa kupitia mtandao na kuwezesha utunzwaji sahihi wa taarifa za wagonjwa, magonjwa, watoa huduma, taarifa za kifedha , usimamizi wa dawa na vifaa tiba .Pia mfumo huu wa GoTHOMIS umekidhi utekelezaji wa sera ya Afya ya kuwajali wazee,watoto,na msamaha kwa Wagonjwa.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Mpango wa Wilaya ni kuhakikisha vituo vyote vya kutolea huduma za Afya **29** vilivyosalia kuwekwa mfumo wa GoTHOMIS mwaka wa fedha 2021/2022. Vituo vyote **42** vya huduma za afya vinatumia vishikwambi vyenye mfumo wa kutoa chanjo kidigitali, mfumo huu unasaidia kuweka takwimu sahihi za majokovu ya chanjo, taarifa za watoto waliozaliwa na wanaopaswa kuchanjwa na kufuatailia mwenendo wa utoaji chanjo katika kituo. Pamoja na mfumo huu kuna kifaa cha Tehama kimewekwa katika jokovu la chanjo, kifaa hiki kinaratibu hali ya ubaridi na kutuma ujumbe mfupi kwa mkuu wa kituo cha huduma za afya pale jokovu linapokuwa na shida ili kuweza kuokoa chanjo.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Vituo vyote vya kutolea huduma za afya vinatoa huduma za wagonjwa wenye kadi za iCHF na NHIF , uhakiki wa kadi za wagonjwa pamoja na kuingiza huduma walizopata kwa ajili ya kudai malipo unafanyika kwa kutumia mifumo ya Tehama.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wilaya ya Newala ina zahanati **13** zinazotumia PoS katika kukusanya mapato,Pia kwa kushirikiana na TAKUKURU tulifanikiwa kuendesha mafunzo kwa waganga wakuu wa zahanati **23** na vituo vya afya **3** na Wahasibu **3** wa vituo vya Afya juu ya matumizi sahihi ya PoS,uwasilishaji wa fedha benki,sheria,uwazi zaidi kwa kubandika bei za dawa kwenye mbao za matangazo,utunzaji wa kumbukumbu za fedha na utoaji wa risiti kwa kila mgonjwa atakayelipia matibabu.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Vituo vyote ndani ya Wilaya vinatumia mfumo wa PlanRep kwa ajili ya kuandaa bajeti na mfumo wa FFARS kwa ajili ya kupokelea Fedha na kutoa fedha kwa ajili ya matumizi mbalimbali ya kituo,mifumo hii imesaidia kurahisisha upangaji wa bajeti,kuthibiti matumizi nje ya mpango,usuluhishi wa taarifa za kifedha na kuongeza uwajibikaji.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba uone mfumo wa Tehama ya Zahanati ya Tupendane.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**MATAALAMU WA AFYA AKIWA ANATOA HUDUMA ZA AFYA KUPITIA KOMPYUTA**



**TAARIFA FUPI YA LISHE KWA KIONGOZI KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA  
MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE  
30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Lishe bora ni msingi wa ukuaji wa mwili na akili na kinga dhidi ya maradhi, Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wilaya ya newala kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile viongozi wa dini, wanasiasa pamoja na wazazi wamekuwa msitari wa mbele katika kuhakikisha utekelezaji wa afua za lishe, Ushiriki wa wananchi katika kuimarisha lishe bora ni mkubwa sana hasa kwenye maeneo ya kutolea huduma za afya na jamii kwa ujumla. kupitia redio newala, nyumba za ibaada, mikutano ya kijiji pamoja na kufanya maazimisho mbalimbali katika jamii kama vile maazimisho ya wiki ya unyonyeshaji, siku ya afya na lishe ya kijiji wananchi wamekuwa tukielimishwa kuhusu lishe na umuhimu wa lishe bora katika familia na jamii kwa ujumla. pamoja na hayo yote wilaya imekuwa ikitenga kiashi cha shilingi elfu moja kwa kila mtoto aliye chini ya miaka mitano ili kusaidia katika utekelezaji wa afua za lishe

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Wilaya ya newala ina jumla ya watoto chini ya miaka mitano **30,703**, wilaya ina wataalamu wa lishe **2**, watoa huduma za afya ngazi ya jamii (WAJA) **332** waliopatiwa mafunzo ya lishe ambao wapo katika ngazi ya vitongoji pamoja na vijiji kwa ajili ya kutoa elimu ya lishe kwa kutembelea kila kaya, sambamba na kutoa rufaa kwa wanaogundulika na dalili zozote za matatizo ya lishe ili kuhakikisha tunatunapambana na janga la utapiamlo.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa mwaka 2020/2021 wilaya ya newala imetekeleza afua za lishe kwa kutoa elimu ya ulishaji kwa wazazi/walezi wenye watoto chini ya miaka miwili kwa **96%**, kutoa matibabu ya utapiamlo kwa watoto chini ya miaka mitano waliobainika na tatizo la utapiamlo **166** kwa **100%**, kutoa matone ya vitamin A ya nyongeza kwa watoto chini ya miaka mitano kwa **99%**, kutoa dawa za kuongeza wekundu wa damu kwa wajawazito **9328** kati ya **9659** sawa na **96.6%**, kutoa elimu kwa wajawazito juu ya umuhimu wa kuwahi kliniki mapema ndani ya miezi mitatu kupitia vituo vyote vya kutolea huduma za afya, redio newala, mikutano ya vijiji, kutoa elimu ya unyonyeshaji ili kuhakikisha kila mtoto anapata lishe bora katika kipindi chote cha siku **1000** za mwanzo ili kuepuka utapiamlo.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Katika kujenga jamii yenye Afya Imara kwa kuzingatia Lishe Bora, Wilaya ya newala imeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kula vyakula mchanganyiko kutoka makundi matano ya vyakula, hasa vyakula vya asili vinavyopatikana katika maeneo yetu, kutumia maji safia na salama, kufanya mazoezi, kutoa elimu ya ulishaji sahihi kwa watoto wadogo na

wachanga, kutumia vyakula vilivyotubishwa kama vile chumvi yenye madini joto, unga wa mahindi, matumizi sahihi ya dawa za kuongeza wekundu wa damu kwa wajawazito, matone ya vitamin A ya nyongeza kwa watoto chini ya miaka 5 na wakina mama baada ya kujifungua.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Wilaya inaendelea kusimamia halmashauri kutenga Tsh. **1000/=** kwa kila mtoto aliye chini ya miaka 5, kupitia halmashauri **2**, wilaya imetenga jumla ya **33,842,104/=** kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe katika bajeti ya 2021/2022 kama ilivyoada. pia wilaya imeandaa vipeperushi vyenye jumbe za lishe, mabango kitita, video pamoja na sauti zinazoelezea umuhimu wa lishe kwa makundi tofauti tofauti, mwongozo wa vyakula mashuleni pamoja na kuweka ajenda ya lishe kuwa ni ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya kisheria vya wilaya.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**


**Mwenge oyeeeeee**

# MAKUNDI YA VYAKULA YANAYOPATIKANA WILAYA YA NEWALA

## NAFAKA, MIZI NA NDIZI MBICHI



## VYAKULA VYENYE ASILI YA WANYAMA NA JAMII YA MIKUNDE



## MATUNDA



## MBOGAMBOGA



## MAFUTA, SUKARI NA ASALI



## **TAARIFA FUPI YA TEHAMA KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Sekta za Uchumi, Mawasiliano, afya na Elimu zimeendelea kuimarika kutokana na matumizi ya TEHAMA katika Wilaya yetu. Mapato yote ya Serikali kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa yanakusanywa kwa kutumia mifumo na Vifaa vya TEHAMA, Jumla ya POS 169 zinatumiwa kukusanya mapato katika Wilaya yetu. Shule zote 150 zilizopo katika wilaya yetu zinatumiwa mifumo ya TEHAMA katika kuchukua mahudhurio (SIS), kuhamisha wanafunzi (PREM/PREMS), kusimamia takwimu za shule (BEMIS) na matumizi ya fedha (FFARS). Pia kati ya vituo vya kutolea huduma za Afya 42, vituo 13 vinatumia mfumo wa GOTHOMIS katika kukusanya mapato, kuhifadhi takwimu na kusimamia dawa na vifaa tiba.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wanafunzi wote wa shule za Msingi na Chuo cha Elimu Kitangali wanapata elimu ya awali juu ya mifumo na matumizi ya TEHAMA. Wananchi wa Newala wanaendelea kupata Elimu juu ya Sheria na Kanuni za TEHAMA kwa kupitia watoa huduma za kifedha, watoa huduma za simu, redio Newala, tovuti za Halmashauri, mitandao ya kijamii, mihadhara na vyombo vya ulinzi na usalama.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Ili kuimarisha Ulinzi na Usalama hasa katika maeneo ya mpaka na msumbiji, Wilaya inaendelea kushirikiana na wizara ya mawasiliano, TCRA na kampuni za mitandao ya simu ili kuhakikisha huduma za uwakika za mawasiliano ya simu na radio. Tahadhari dhidi ya utapeli wa kimtandao inaendelea kutolewa na polisi, taasisi za kibenki na makampuni ya simu. Wakulima wa Korosho wananufaika na matumizi ya TEHAMA katika kutafuta masoko na malipo yao kufanyika kwa haraka na uhakika kwa kutumia taasisi za kifedha/benki.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wananchi wa Newala wamechangamkia fursa za TEHAMA kwa kushiriki katika maduka mtandao, kutuma na kupokea fedha kutumia simu zao. Uwepo wa maduka ya simu, mawakala wa CRDB, NMB, Mpesa, TiGO pesa, Halopesa, Airtel money, mafundi wa kompyuta na simu, huduma za intaneti na maduka ya picha mnato katika Wilaya yetu ni mwikotikio chanya wa wananchi katika kutumia fursa na kuweza kujijiri.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba utembelee na kukagua Banda letu.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

## MATUMIZI YA TEHAMA



**MKUSANYA MAPATO STENDI YA MABASI  
AKITUMIA POS**



**AFISA ELIMU AKIMUHAMISHA MWANAFUNZI  
KATIKA MFUMO**



**WANAFUNZI WA CHUO CHA UALIMU KITANGALI  
WAKIPATIWA MAFUNZO YA TEHAMA.**



**KAMANDA WA POLISI AKITOA MAFUNZO JUU  
YA SHERIA ZA MITANDAO**

**TAARIFA FUPI YA SHUGHULI ZA MAPAMBANO DHIDI YA MAAMBUKIZI YA  
VVU/UKIMWI KWA KIONGOZI KWA MBIO MALAALUM ZA MWENGE WA UHURU  
KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Ujumbe huu umebeba kaulimbiu "**MSHIKAMANO WA KITAIFA TUWAJIBIKE KWA PAMOJA**"  
" Mwenge wa uhuru kwa mwaka 2021, unatukumbusha kuwa afya zetu ndio mtaji wetu, hivyo tuchukue hatua ya kupima VVU/UKIMWI mara kwa mara ili kujua hali zetu kisha tuchukue hatua stahiki za kupambana na VVU/UKIMWI. Hali ya Maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa halimashauri ya Mji Newala imepungua kutoka **2%** mwaka 2019 hadi **1.78%** mwaka 2021. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile **USAID Boresha Afya, NEW-NGONET, MKAPA FOUNDATION, NACOPHA, Viongozi wa kisiasa** na **Viongozi wa dini**, inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusiana na njia za kujikinga na maambukizi ya VVU/UKIMWI kwa wenza, vijana, na watoto chini ya miaka 15 kupitia radio Newala, Vikao vya afya ya Msingi na vikao vya kisheria ngazi ya Vijiji, Pia inaendelea kusambaza kondomu katika maeneo mbalimbali sambamba na kutoa elimu ya matumizi sahihi ya kondomu. Aidha halmashauri inaendelea kuwahudumia watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kwa kuwapatia matibua ya ARVs kulingana na miongozo na hili linaenda sambamba na kutoa elimu juu ya kuendelea kujikinga ili wasipate maambukizi mapya.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Halmashauri inaendelea kufanya usimamizi elekezi kwenye vituo vinavyotoa huduma za **CTC, HTS, STI, TB/HIV** na **CBHS**. Kwa mwaka 2020/ 2021, Jumla ya watu **7726** kati yao wanaume ni **3137** na wanawake ni **4589** wamepima afya zao (VVU/UKIMWI) kupitia huduma za **HTS**, kati yao **138** waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU/UKIMWI ambapo wanaume walikuwa ni **56** na wanawake ni **82**. Halmashauri ina vituo **12** vinavyotoa matibabu ya dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI (ARVs) ambapo jumla ya wateja **2883** kati yao wanawake ni **2091** na wanaume **792** wamesajiliwa kwenye huduma, na jumla ya akinamama **42** wajawazito na wanaonyonyesha wanaishi na **VVU/UKIMWI** wamesajiliwa kwenye huduma za **PMTCT**.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Halmashuri inaendelea kutoa huduma za wagonjwa majumbani (**CBHS**), ambapo WAVIU **2001** wanaendelea kutembelewa na kuhudumiwa kupitia mfumo wa huu .

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba utembelee na kukagua Banda letu.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge oyeeeeeeeeeeee!**

**TAARIFA FUPI YA SHUGHULI ZA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA  
KWA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL  
MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

Ujumbe huu umebeba kauli mbiu **“Ziro malaria Inaanza na Mimi- Chukua hatua kuitokomeza”**.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Ugonjwa wa malaria una athari kubwa katika maendeleo ya wananchi, athari hizo ni pamoja na mahudhurio hafifu ya wanafunzi mashuleni, upoteaji wa nguvu kazi ya taifa, gharama za matibabu na kukatisha maisha na ndoto za mama wajawazito na watoto.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Hali ya maambukizi ya malaria imepungua kutoka **37.3% 2019** hadi **35% 2020**, kupungua kwa kiwango cha malaria kimetokana na wilaya kutekeleza afua za kinga na tiba ya malaria kama kudhibiti mbu waenezo malaria kwa kuhamasisha wananchi kutumia vyandarua vyenye dawa, kusafisha mazingira, kufanya uchunguzi wa vimelea vya malaria kwa kutumia kipimo cha mRDT na hadubini, matumizi ya dawa mseto kwa wagonjwa waliobainika kuwa na vimelea vya malaria, kinga ya SP kwa wajawazito, kugawa vyandarua vyenye dawa kwa wajawazito, watoto chini ya mwaka mmoja na wanafunzi na kuua viluilui vya mbu kwa kufanya upulizaji wa viudadu kwenye mazalia ya mbu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa mwaka **2019/2020**, Jumla ya vyandarua **37,577** viligawiwa kwa wanafunzi kama njia ya kupeleka katika jamii, asilimia **99.7%** ya Wajawazito na asilimia **99.0%** ya watoto waligawiwa vyandarua kliniki. Wajawazito waliohudhuria kliniki walikuwa **20,680** na walipata kinga ya **SP** dozi ya **3** sawa na asilimia **92.1%**. Pia mazalia ya mbu **84** yalitambuliwa katika kata **5** na yote yalipuliziwa viudadu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Wananchi wa Newala katika mapambano ya malaria wanaendelea kuelimishwa kufanya usafi wa mazingira na kuharibu mazalia ya mbu, matumizi sahihi ya vyandarua ikiwemo kulala ndani ya vyandarua kila siku, kufua na kushona vyandarua, kuwahi vituo vya kutolea huduma za afya pale wanapohisi dalili za malaria, matumizi sahihi ya dozi **3** za SP, kuwahi kliniki kwa mama wajawazito, kutumia dawa mseto na kumaliza dozi.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba utembelee na kukagua Banda letu.

Asante sana kwa kunisikiliza

**ASANTE KARIBU TENA NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

## PICHA ZINAZOONYESHA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA



**TAARIFA FUPI YA MADAWA YA KULEVYA KWA KIONGOZI WA MBIO MAALUM ZA  
MWENGE WA UHURU KITAIFA KWA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI  
TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Dawa za kulevya ni kemikali zitokanazo na mimea na madini ambayo ni malighafi muhimu kwa mahitaji mengine ya mwanadamu. Dawa zitumikapo mwilini huathiri ubongo wa mtumiaji na kumsababishia mtumiaji kuwa na matendo, hisia, fikira na muonekano tofauti na matarajio ya jamii. Dawa hizi huingia mwilini kwa kunywa / kula, kuvuta na kujidunga sindano. Dawa za kulevya ziko ambazo zimeruhusiwa kisheria kama tumbaku, na pombe na dawa zisizoruhusiwa kisheria ni pamoja na bhangi, mirungi, cocaine, heroin, dawa tiba zenye asili ya kulevya na viyeyusi (gundi na petrol). Pia, kuna dawa zinazoruhusiwa kwa matumizi ya Hospitali kama Valium, Pethedine, Morphine n.k

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

**MADHARA**

Matumizi na biashara ya madawa ya kulevya yana athari kiuchumi, kimazingira, kiusalama, kiafya na kijamii. Athari hizo ni pamoja na kupungua kwa nguvukazi; kutupa ovyo sindano/vifaa vilivyotumika; matendo ya uharifu, ubakaji na ajali; kuzorota kwa afya hasa vijana ambao wanategemewa katika uzalishajimali; kuchangamka sana kusiko kawaida baada ya matumizi ya dawa hizo; kuchanganyikiwa kiakili/kuwehuka; Kupoteza kumbukumbu; kupelekea magonjwa ya akili, moyo, mapafu, ini, kiharusi, magonjwa ya ngozi na utapiamlo; na mmomonyoko wa maadili;

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

**MAPAMBANO DHIDI YA DAWA YA KULEVYA**

Wilaya imefanikiwa kupunguza makosa ya madawa ya kulevya kutokana na misako/doria za mara kwa mara pamoja na utoaji elimu kwa jamii kupitia vipindi vya redioni; Kupunguza kwa kesi za mashambulio na kuleta utulivu na amani katika jamii; Kupunguza kwa idadi ya mahabusu/wafungwa wanaotokana na kesi za madawa ya kulevya. Hadi sasa, Wilaya kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imeweza kukamata jumla ya kilo **43** za bhangi, kilo **8** Heroine, mashamba **2** ya bangi na kuteketeza. Aidha, watuhumiwa **34** walikamatwa na kufikishwa mahakamani ambapo kesi **28** zimepata mafanikio kwa watuhumiwa kufungwa jela na kulipa faini, na kesi **3** bado ziko mahakamani.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

**CHANGAMOTO**

Katika kukabiliana na matumizi/biashara ya dawa za kulevya, wilaya imepata changamoto zifuatavyo;

- Uelewa mdogo kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na madawa ya kulevya.

- Uchache wa rasilimali watu (Askari) katika kukabiliana na matumizi ya madawa ya kulevya kulingana na ukubwa wa eneo tulilopo.
- Uhaba wa rasilimali vifaa.
- Wahalifu wengi kubadilisha mara kwa mara **mbinu** za usafirishaji wa madawa ya kulevya

## **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

### **Muono mbele**

Jeshi la polisi limejipanga kuendelea na mapambano ya madawa ya kulevya kwa kutoa elimu kwa jamii kuhusu madhara yatokanayo na madawa ya kulevya, kufanya misako/ doria ili kupunguza/kumaliza kabisa uuzaji na matumizi ya madawa ya kulevya. Aidha, wilaya inawaasa wananchi wote kutojihusisha na matumizi/biashara ya dawa za kulevya.

Nawasilisha tafadhali.

**ASANTE, KARIBU NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**TAARIFA FUPI YA BANDA LA TAKUKURU (W) NEWALA KWA KIONGOZI KWA MBIO  
MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI  
TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

TAKUKURU (W) Newala inaendelea kutekeleza Majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007 kama ifuatavyo:-

- Kupitia na kuchambua sheria , mifumo ya utendaji, mifumo ya utoaji huduma kwa lengo la kubaini kama kuna mianya au viashiria vya uwepo wa rushwa.
- Kutoa ushauri wa namna ya kuzuia na kupambana na rushwa ndani ya sekta ya umma na binafsi.
- Kuelimisha umma kuhusu dhana ya rushwa na madhara yake.
- Kuhamasisha wananchi ili watambue ubaya wa rushwa na hatimaye wajiunge katika vita dhidi ya rushwa.
- Kufuatilia thamani ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya nchi.
- Kujenga ushirikiano na taasisi mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha vita dhidi ya rushwa inafanikiwa.
- Kupokea na kuchambua malalamiko yanayohusu vitendo vya rushwa na makosa yaliyoainishwa kwenye sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa.
- Kuchunguza tuhuma zilizopokelewa kwa lengo la kupata ushahidi wa kuthibitisha au kutothibitisha tuhuma zilizopokelewa.
- Kuwashitaki mahakamani watuhumiwa kwa mujibu wa sheria.
- Na kwa kibali cha mahakama kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia za rushwa.



- *Pichani (kushoto) Afisa wa TAKUKURU Wilaya Newala Bi FIDES DIDAS akielimisha wanafunzi wa shule ya sekondari KIUTA juu madhara ya rushwa na hatua za kuchukua ili kuitokomeza (kulia )ni wanafunzi hao wakifuatilia elimu hiyo.*

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

TAKUKURU Newala kwa kushirikiana na wadau inaendelea kupambana na vitendo vya rushwa ambapo kwa kipindi cha Agosti 2019 hadi Agosti 2021, tumeichunguza na kukamilisha majalada tisa **(09)**. Uchunguzi ulihusu manunuzi ya umma, ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, afya, elimu na vyama vya ushirika. Idadi ya kesi zilizofunguliwa ni moja **(01)** na fedha zilizookolewa ni shilingi milioni mia mbili themanini na nane laki tano tisini na tatu na mia tatu sabini na tisa (288,593,379/=). Aidha TAKUKURU imefanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za serikali katika miradi ya maendeleo ishirini na tano **(25)** yenye thamani ya shilingi bilioni tatu milioni mia nne kumi na tano na elfu saba mia nne kumi na mbili (3,415,007,412/=) kutoka katika sekta za afya, maji, elimu na ujenzi wa miundombinu.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Katika miradi yote iliyofuatiliwa haina upungufu mkubwa, ambapo wahasika wameelimishwa na kushauriwa namna ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo ili iwiane na thamani ya fedha (value for money). Aidha, kwa kipindi tajwa, tumetoa elimu kwa Umma kuhusu sababu za rushwa na umuhimu wa kuzingatia maadili kupitia vikao na mikutano ya Watumishi wa Umma, Vyama vya Ushirika, Kamati za usimamizi wa Miradi ya Ujenzi ngazi ya vijiji na Kata na wananchi wote kupitia mikutano; ambapo katika kipindi cha Agosti 2019 hadi Agosti 2021 tumeendesha semina sabini na moja **(71)** na kufanya mikutano hamsini na nne **(54)**, TAKUKURU imeendelea kuimarisha na kuelimisha Vilabu vya Wapinga Rushwa mia arobaini na saba **(147)** vilivyopo katika **shule za msingi** mia moja kumi na sita **(116)**, **sekondari** ishirini na nane **(28)** na **vyuo** vitatu **(3)**. Aidha, tumefanya **maonesho** manne (4) na kwa kutumia redio Newala ambapo jumla ya vipindi kumi **(10)** vya mapambano dhidi ya rushwa vimerushwa katika kipindi tajwa.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwenye ujumbe wa kudumu wa Mapambano Dhidi ya Rushwa wa mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 unasema **"Kupambana na Rushwa na Jukumu ni Langu"** TAKUKURU Wilaya ya Newala inaendelea na jukumu la kuishirikisha jamii, makundi mbalimbali na wadau wote kwa ujumla katika mapambano dhidi ya rushwa. Pia, Kuelimisha Wananchi wayajue madhara yatokanayo na Rushwa na kusihhi watu wote kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, Kanuni, taratibu na miongozo ili kuiletea Jamii ya Watanzania Maendeleo kuelekea uchumi wa kati.

### **Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru**

Kwa heshima na taadhima tunakuomba utembelee na kukagua Banda letu.

**Asante sana kwa kunisikiliza.**

**Mwenge Oyeeeeeeee!**

**FIDES DIDASI**

**TAKUKURU WILAYA NEWALA**

**TAARIFA NA TAKWIMU MUHIMU KUHUSU WATU WENYE ULEMAVU WILAYA YA  
NEWALA KWA KIONGOZI KWA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU KITAIFA  
LUTENI JOSEPHINE PAUL MWAMBASHI TAREHE 30/08/2021**

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa**

Wilaya ya Newala inaendelea kufanya utambuzi na kuthamini kundi maalumu la watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria Na. 9 ya mwaka 2010 na sera ya Taifa ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2004 ibara ya 1.2. Wilaya inaendelea na kufanya utambuzi ambapo Hadi 30 August 2021 Wilaya imetambua jumla ya watu wenye ulemavu **1,894** kutoka kwenye kata 34 kati ya kata 38, vijiji 123 kati ya vijiji 155 na mitaa 11 (kati yao watu wazima ni **1,591** na watoto **303**). Wilaya imebaini watu wenye walemavu wa viungo ni **797**, wasioona **415**, Viziwi **72**, Watu wenye ulemavu wa ngozi **143**, Bubu **47**, Akili/Usonji **420** kama inavyoonesha katika jedwali lifuatalo.

WILAYA	VIUNGO			MACHO			NGOZI			AKILI/USONJI			VIZIWI			BUBU			JUMLA KUU		
	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML	ME	KE	JML KUU
MJI	163	148	<b>311</b>	72	80	<b>152</b>	18	21	<b>39</b>	135	118	<b>253</b>	11	9	<b>20</b>	13	7	20	412	383	795
WILAYA	262	224	<b>486</b>	121	142	<b>263</b>	59	45	<b>104</b>	94	73	<b>167</b>	16	36	<b>52</b>	14	13	27	556	533	1099
JUMLA	425	372	<b>797</b>	193	222	<b>415</b>	77	66	<b>143</b>	229	191	<b>420</b>	27	45	<b>72</b>	27	20	47	978	916	1894

**NB** Kiambatisho.....kinaonesha Mchanganuo wa waliotambuliwa kwa watoto chini ya miaka 18 na watu wazima kwa kila kijiji/mtaa kijinsia.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa;**

Wilaya inaendelea kutekeleza Afua stahiki kwa watu wenye ulemavu, kwa kipindi cha 2020/21 Wilaya imeweza kuunda kamati za watu wenye ulemavu **205** kati ya hizo **155** ziko ngazi ya vijiji, **11** ngazi ya mtaa **38** ngazi ya kata na **1** ngazi ya Wilaya, imetoa msamaha wa matibabu kwa watu wenye ulemavu **179**, imewapatia mafuta maalum chupa **65** watu wenye ulemavu wa ngozi, imetoa vifaa saidizi baiskeli mwendo **45** kwa watoto na watu wazima wenye ulemavu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa;**

Wilaya inaendelea kutenga fedha za Vifaa vya Ujifunzaji na ufundishaji kwa watoto wanaosoma elimu jumuishi katika shule za msingi na sekondari. Kwa sasa idadi ya watoto wanaosoma elimu jumuishi imeongezeka kutoka **52** mwaka 2020 hadi **163** mwaka 2021 ongezeko hili limetokana na utambuzi uliofanyika na utoaji wa vifaa saidizi.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa;**

Wilaya inaendelea kuwa wezesha watu wenye ulemavu kiuchumi kupitia vikundi vya wajasiriamali. Ambapo kwa kipindi cha miaka 2 ( 2019/20 - 2020/21, Wilaya imetoa mikopo wenye thamani ya Tsh; **29,900,000/=** kwa vikundi 15 vyenye wanachama **124**. Wilaya inaendelea kutenga 2% ya mapato halisi ya Halmashauri ambapo kwa mwaka 2021/22 Wilaya itenga Tsh. **46,833,240/=** kwa ajili ya kuwezesha vikundi vya watu wenye ulemavu.

**Ndugu kiongozi wa mbio maalum za mwenge wa uhuru Kitaifa;**

Inaendelea kuwezesha watu wenye ulemavu kuhudhuria maadhimisho, makongamano na warsha mbalimbali zinazo walenga. Tunaipongeza serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kutekeleza afua za watu wenye ulemavu.

**ASANTE KARIBU TENA NEWALA.**

**Mwenge wa Uhuru Oyee!!!**

**PICHA YA WATU WENYE ULEMAVU WAKIWA WANA WEZESHA VIFAA**



**MHE. GEORGE H. MKUCHIKA MBUNGE WA JIMBO LA NEWALA MJI AKIKABIDHI BAIKLEI ZA WALEMAVU**



**WANAFUNZI WAKIKABIDHIWA BAIKELI ZA WALEMAVU**

# **RISALA YA UTII YA WANANCHI WA NEWALA KWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN WAKATI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU TAREHE 30, AGOSTI, 2021**

## **1.0 UTANGULIZI**

### **Mheshimiwa Rais,**

Sisi Wananchi wa Newala tupatao **205,492** kwa shangwe, heshima na taadhima leo, tumeupokea na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru wa Mwaka 2021. Wilaya yetu ina Tarafa **6**, Kata **38**, mitaa **11**, Vijiji **155**. Wilaya imekimbiza Mwenge wa Uhuru katika tarafa **2**, kata **10** na vijiji **23** kwa umbali wa kilomita **81** hadi eneo la makabidhiano

### **Mheshimiwa Rais,**

Wananchi wa Newala tunatambua kuwa, Mwenge wa Uhuru ni ishara ya kuleta **Maendeleo, Uzalendo, Umoja, Mshikamano** na **kudumisha Amani** miongoni mwa Watanzania katika kusukuma shughuli za maendeleo ya Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi. Sisi wananchi wa Newala kwa heshima kubwa, tunawakaribisha wakimbiza Mwenge wa Uhuru na kuwapa pole kwa safari ndefu.

### **Mheshimiwa Rais,**

Mwenge wa Uhuru mwaka 2021, umekimbizwa ukiwa na ujumbe muhimu uliojikita katika kutuhamasisha sisi wananchi wa Newala kutumia TEHAMA chini ya kauli mbiu isemayo **"TEHAMA ni msingi wa Taifa endelevu; itumie kwa usahihi na uwajibikaji"**. Pamoja na kauli mbiu hii, mbio za Mwenge wa uhuru, umeendelea kutuhamasisha kuhusu **Umuhimu na uzingatiaji wa Lishe bora, Mapambano dhidi ya Rushwa, VVU/UKIMWI, Matumizi ya Dawa za kulevya na Malaria.**

### **Mheshimiwa Rais,**

Hali ya ulinzi na usalama ni shwari wananchi wanaendelea na utekelezaji wa majukumu yao ya kijamii na kiuchumi.

## **2.0 UTEKELEZAJI WA UJUMBE WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021**

### **Mheshimiwa Rais**

Wananchi wa Newala kwa heshima na taadhima tunaomba kuwasilisha kwako muhtasari wa utekelezaji wa ujumbe wa Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2021 kama ifuatavyo:

### **2.1 TEHAMA NI MSINGI WA TAIFA ENDELEU; ITUMIE KWA USAHIHI NA UWAJIBIKAJI.**

#### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya inaendelea kutoa elimu kwa Wananchi juu ya sheria, kanuni, Faida na Madhara ya matumizi ya TEHAMA katika utoaji huduma za kiuchumi, kijamii, Kisiasa, Mila na desturi kupitia Redio Newala, mihadhara, na mikutano. Aidha, Wilaya inatumia mfumo TEHAMA katika ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali kupitia (Posta, TRA, Halmashauri, Maji, Ardhi, Nishati, Polisi) na kusajili watumiaji wa huduma mbalimbali kama wakulima, usajili wa wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu, vitambulisho vya Taifa (NIDA), RITA na utoaji wa huduma za Afya (GoTHomis).

### **Mheshimiwa Rais,**

Wananchi wanaendelea kutumia Fursa ya TEHAMA katika shughuli za kiubunifu, Masoko, Mitaji na Ajira ambapo hadi sasa Wilaya ina mawakala **125** wa huduma za kifedha kwa njia ya mitandao ya simu na benki (M-Pesa, Tigo pesa, Halopesa, Airtelmoney, NMB, CRDB), ina maduka ya vifaa vya kidigitali, mafundi simu, huduma za intaneti café na huduma za stationery pamoja na picha.

## **2.2. MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA.**

Ujumbe huu umebeba kauli mbiu **“Kupambana na Rushwa ni Jukumu langu”**

### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya inaendelea kupambana na vitendo vya rushwa ambapo kwa kipindi cha 2019/20 hadi Juni 2021, Wilaya imechunguza na kukamilisha majalada **9**. Uchunguzi ulihusu manunuzi ya umma, ukusanyaji wa maduhuli ya serikali na vyama vya ushirika. Idadi ya kesi zilizofunguliwa ni **1** na fedha zilizookolewa ni Tsh. **288,593,379/=**. Aidha Wilaya imefanya ufuatiliaji wa matumizi ya fedha kwa miradi ya maendeleo **25** yenye thamani ya Tsh. **3,415,007,412/=**, miradi yote iliyofuatiwa haina upungufu mkubwa, ambapo wameelimishwa na kushauriwa namna ya kuboresha utekelezaji wa miradi hiyo ili iwiane na thamani ya fedha (value for money).

### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya inaendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu sababu za rushwa na umuhimu wa kuzingatia maadili kupitia vikao vya Watumishi wa Umma, Vyama vya Ushirika, Kamati za usimamizi wa Miradi ya Ujenzi ngazi ya vijiji, kata na wananchi wote. Ambapo kwa kipindi cha 2019/20 hadi Juni 2021 Wilaya imeendesha vipindi **10** vya redio, semina **71**, mikutano **54**, kuimarisha na kufuatilia Vilabu **147** vya Wapinga Rushwa kati ya hivyo **116** viko shule za msingi, **28** sekondari na **3** vyuo na kufanya maonesho **4** kuhusu mapambano dhidi ya Rushwa.

### **Mheshimiwa Rais,**

Ushiriki wa wananchi katika mapambano dhidi ya rushwa ni mkubwa ambapo wananchi wanaendelea kukumbushwa, wajibu wao katika usimamizi na utekelezaji wa miradi, kujitolea, kutojikusisha na vitendo vya Rushwa na kuwa tayari kutoa taarifa pale wanapobaini uhalifu kwenye ofisi husika au kwa kutumia namba **113**.

## **2.3 Elimu sahihi juu ya Dawa za Kulevya Huboresha Huduma kwa Waraibu: Chukua hatua.**

### **Mheshimiwa Rais,**

Katika kupambana na dawa za kulevya, wilaya kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama imeweza kukamata jumla ya kilo **43** za bangi, kilo **8** Heroine, mashamba **2** ya bangi na kuteketeza, aidha watuhumiwa **37** walikamatwa. kati ya waliokamatwa watuhumiwa **34** walifikishwa mahakamani ambapo kesi **28** zimepata mafanikio kwa watuhumiwa kufungwa jela na kulipa faini, kesi **3** bado ziko mahakamani.

### **Mheshimiwa Rais,**

Watumiaji wengi wa dawa za kulevya ni vijana ambao ni nguvu kazi ya Taifa. Wilaya, kwa kushirikiana na wadau, inaendelea kuwaelimisha vijana na wazazi kuhusu wajibu wao katika

kupambana na dawa za kulevya; Jamii ina elimishwa kutojikusisha katika biashara, matumizi na kilimo cha madawa ya kulevya, kujiepusha na vitendo vya unyanyapaa dhidi ya waathirika, Kuwasaidia na kuwapa huduma za kimatibabu, lishe na kuwajengea nguvu za kiuchumi vijana wetu. Wilaya kwa kushirikiana na wadau inaendelea kuelimisha wananchi kujenga jamii yenye maadili kwa kuwasikiliza, kuwajali na kuwalea vijana. Aidha, Wilaya inasisitiza jamii kutoa taarifa kwa wakati za watu wanaojikusisha na dawa za kulevya kwenye vyombo vya ulinzi na usalama.

## **2.4 UMUHIMU NA UZINGATIAJI WA LISHE KWA AFYA;**

Chini ya Kauli mbiu isemayo **“Tujenge jamii yenye Afya Imara kwa kuzingatia Lishe bora”**.

### **Mheshimiwa Rais**

Lishe bora ni msingi wa ukuaji wa mwili na akili ya mtoto na kinga dhidi ya maradhi. Wilaya ina watoto chini ya miaka mitano **30,703** kati yao watoto wenye udumavu **9,211**, wenye ukondefu ni **491** na watoto wenye uzito pungufu **3,070**. Wilaya ina wataalam wa lishe **2**, kamati za lishe **2** na watoa huduma za afya ngazi ya jamii (WAJA) **332** Wilaya imetenga jumla ya Tsh. **33,843,104/=** kwa ajili ya kutekeleza afua za lishe katika bajeti ya 2021/2022.

### **Mheshimiwa Rais;**

Kwa 2020/21 Wilaya imetekeleza afua za lishe kama ifuatavyo; vituo vilivyofanyiwa usimamizi shirikishi **45**, wajawazito **9,328** walipewa vidonge vya FeFO kati ya **9659**; Watoto chini ya miaka 5 waliopata matibabu ya utapiamlo mkali **166** na waliopewa matone ya vitamin A ni **30,396** sawa na **99%**, Vikao vya kamati ya Lishe vilivyofanyika **4** na **96%** ya wazazi/walezi wenye watoto wa miezi 0-23 walipewa elimu ya ulaji.

### **Mheshimiwa Rais**

Wilaya inaendelea kuelimisha wananchi juu umuhimu wa kula milo kamili na kutumia maji safi na salama. Wilaya inaendelea kutoa elimu ya ulishaji sahihi wa watoto chini ya miaka 5, ulaji unaofaa, kufanya mazoezi, kutumia vyakula vilivyorutubishwa kama chumvi, matumizi sahihi ya vidonge vya kuongeza damu kwa wajawazito na matone ya Vitamin A kwa watoto chini ya miaka **5**. Kuhamasisha jamii kulima vyakula na ulaji wa mazao yenye viini lishe kama viazi lishe, mahindi lishe, maharage nk

## **2.5 MAPAMBANO DHIDI YA MALARIA.**

Ujumbe huu unabeba kauli mbiu **“Ziro malaria Inaanza na Mimi- Chukua hatua kuitokomeza”**.

### **Mheshimiwa Rais,**

Ugonjwa wa Malaria una athari kubwa katika maendeleo ya wananchi, athari hizo ni pamoja na mahudhurio hafifu ya wanafunzi shuleni, upoteaji wa nguvukazi ya taifa, gharama za matibabu na kukatisha maisha na ndoto za wananchi hasa mama wajawazito na watoto.

### **Mheshimiwa Rais**

Hali ya maambukizi ya malaria imepungua kutoka **37.3%** 2019 hadi **35%** 2020, kupungua kwa kiwango cha malaria kumetokana na Wilaya kutekeleza afua za kinga na tiba ya malaria kama

kudhibiti Mbu waenezo Malaria kwa kuhamasisha wananchi kutumia vyandarua vyenye dawa, kusafisha mazingira na kuuwa viluili vya mbu; Kufanya uchunguzi na matibabu ya malaria kwa kutumia kipimo cha **mRDT** au hadubini, matumizi ya dawa mseto kwa wagonjwa waliobainika kuwa na vimelea vya malaria, kuwapa watoto na wajawazito vyandarua vyenye dawa na vidonge wakati wa ujawazito. Aidha, Wilaya inaendelea kutekeleza afua za malaria na kuwasisitiza wananchi kuwahi vituo vya kutolea huduma za afya pale wanapojihisi dalili ya malaria, matumizi sahihi ya dozi **3** za **SP**, kuwahi kliniki kwa mama wajawazito na kutumia dawa mseto.

## **2.6 MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI:**

Ujumbe huu umebeba kaulimbiu **“Mshikamano wa Kitaifa tuwajibike kwa pamoja”**.

### **Mheshimiwa Rais,**

Afya zetu ndio mtaji wetu, hivyo tuchukue hatua ya kupima VVU mara kwa mara ili kujua hali zetu na kuchukua hatua stahiki za kupambana na maambukizi ya VVU na UKIMWI. Wilaya kwa kushirikiana na wadau (**USAID Boresha Afya, NEWNGONET, SHIDEFA, Viongozi wa kisiasa na Viongozi wa dini**) inaendelea kutekeleza mkakati wa **4** wa kudhibiti UKIMWI kwa lengo la kupunguza maambukizi mapya ya VVU na vifo vinavyohusiana na UKIMWI. Wilaya inaendelea kupima, kutoa huduma za ARV kutokomeza unyanyapaa na ubaguzi kwa watu wanaoishi na VVU. Hali ya maambukizi mapya ya VVU/UKIMWI imepungua kutoka **2.5%** mwaka 2019 hadi **1.14%** Agosti 2021.

### **Mheshimiwa Rais**

Mwaka 2020/21 jumla ya watu **30,169** waliojitokeza kupima kwa hiari, kati yao wanaume **11,887** na wanawake **18,282**. Waliobainika kuwa na maambukizi mapya ya VVU ni **345** kati yao wanaume ni **116** na wanawake **229**. Wilaya ina endelea kutoa huduma za matibabu ya dawa za kufubaza makali ya VVU/UKIMWI (ARVs) kupitia vituo **22** kwa wateja **4,420** kati yao wanaume **1,267** na wanawake **3,153**. Aidha, Huduma za PMTCT kwa akina mama wajawazito na wanaonyonyesha **105** wanaoishi na VVU/UKIMWI na huduma za wagojwa majumbani (CBHS) kwa WAVIU **3001** zinaendelea kutolewa. Wilaya inaendelea na kuwahamasisha wananchi kubadili tabia, kuimarisha huduma za kitabibu na kuhamasisha matumizi sahihi ya kondom.

## **3.0 MAFANIKIO YA KISEKTA KUANZIA MWAKA 2020 HADI KUFIKIA SASA 2021**

### **3.1 Mafanikio ya sekta ya elimu kuanzia mwaka 2020 hadi 2021**

### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ina shule za msingi **120** kati yake 1 ni ya sekta binafsi, zenye jumla ya wanafunzi **42,830** (Wavulana **21,191** na Wasichana **21,639**), shule za sekondari **26** zenye jumla ya wanafunzi **12,112** (wasichana **6,716** na wavulana **5,396**) na vyo **3**. Idadi ya walimu imeongezeka kutoka **686** mwaka 2020 hadi **733** mwaka 2021 kwa shule za msingi na kutoka **523** hadi **433** kwa sekondari. Uandikishaji wa wanafunzi unaendelea kuongezeka kutoka **5,272** mwaka 2020 hadi **5,334** mwaka 2021 kwa darasa la awali, **6,024** mwaka 2020 hadi **6,140** mwaka 2021 kwa darasa la I na **5411** mwaka 2020 hadi **5764** mwaka 2021 kwa kidato cha I. Ufaulu wa wanafunzi

wa kidato cha IV umeongezeka kutoka **89%** mwaka 2019 hadi **90.5%** mwaka 2020 na ufaulu wa wanafunzi wa kidato cha VI kwa miaka yote umeendelea kuwa **100%**. Mafanikio mengine ya elimu ni katika ujenzi wa miudombinu na samani;

WILAYA/SEKTA	MADARASA		MADAWATI/VITI NA MEZA		MAABARA		MATUNDU YA VYOO		NYUMBA ZA WALIMU		MABWENI	
	2020	2021	2020	2021	2020	2021	2020	2021	2020	2021	2020	2021
ELIMU MSINGI	824	853	14,713	15,247	-	-	1,197	1,240	276	279	-	-
ELIMU SEKONDARI	392	433	15,151	16,920	46	72	610	621	186	186	17	19
Jumla	1,216	1,286	29,864	32,167	46	72	1,807	1,861	462	465	17	19

N.B: 2020 = kutoka mwaka na 2021= hadi mwaka

Wilaya ina ishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kutenga na kuleta fedha kwa ajili ya Utoaji wa Elimu bila malipo, ujenzi wa miundombinu ya elimu, vitabu, vifaa vya maabara upandishaji madaraja walimu **529** na magari **2** kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji.

### 3.2 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA AFYA

#### Mheshimiwa Rais,

Wilaya ina vituo vya kutolea huduma za afya **45**. Kati ya hivyo, ina Hospitali **1** ya Serikali, Vituo vya afya **5** (**1** cha binafsi), zahanati **39** (**37** ni za serikali, **1** ya kikosi cha magereza na **1** ni ya binafsi). Wilaya ina watumishi wa sekta ya afya **345**. Upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya ni wastani wa **98%** kwa kuzingatia dawa muhimu (Tracer Medicine). Aidha Wilaya inaendelea na ujenzi, ukamilishaji na kuomba usajili wa vituo vya afya **2** na zahanati **12** mpya za vijiji. Wilaya ina ishukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kutenga na kuleta fedha za ujenzi wa miundombinu, upandishaji madaraja watumishi wa afya **68** na gari moja la kubebea wa wagonjwa. Wilaya inaendelea na kampeni ya huduma ya chanjo ya UVIKO-19 ambapo hadi sasa jumla ya chanjo **2,157** kati ya **3,900** sawa na **81%** imetolewa.

#### Mheshimiwa Rais,

Wilaya ina tekeleza Afua stahiki kwa watu wenye ulemavu, kwa kuunda kamati **205** ngazi ya kata, vijiji na mitaa, imetoa msamaha wa matibabu **179**, mafuta maalum chupa **65** kwa watu wenye ulemavu wa ngozi, vifaa saidizi baiskeli mwendo **45**. Aidha, imetambua watu wenye ulemavu **1,894** kati yao watu wazima ni **1,591** na watoto **303**, imetenga fedha za Vifaa vya kujifunzia na kufundishia, imeongeza idadi watoto wanaosoma elimu jumuishi, kutoka **52** mwaka 2020 hadi **163** mwaka 2021, imewezesha mikopo yenye thamani ya Tsh; **29,900,000/=** kwa vikundi **15** na imetenga sh. **46,833,240/=** mwaka 2021/22.

### 3.3 MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA MAJI

#### Mhe. Makamu wa Rais;

Wilaya ya Newala inahudumiwa na mamlaka ya Majisafi na usafi wa Mazingira – Makonde. Mamlaka hii ina skimu **5**, Skimu **3** zinafanyakazi na zina uwezo wa kuzalisha maji wastani wa lita

**5,700,000** za maji kwa siku wakati mahitaji halisi ya maji ni lita **9,700,000** za maji kwa siku. Wastani wa upatikanaji wa huduma ya maji ni **58%**. Wilaya ina mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika ngazi ya kaya, taasisi binafsi na umma **59,185**. Hata hivyo mfumo huu huhifadhi maji kwa muda wa miezi 4 tu. Aidha, Wilaya inaendelea na ujenzi wa miradi ya maji Chitandi, Miyuyu na Mnima, Mchemo, Chiule, Mtongwele, Mnolela na ukarabati wa laini ya umeme kutoka chanzo cha maji Mitema.

#### **4.0 KILIMO**

##### **Mheshimiwa Rais,**

Wananchi wa Newala wana Mahitaji ya chakula kwa mwaka tani **56,686.50** za wanga (Wanga na nafaka) na tani **10,685.6** za jamii ya mikunde. Kwa mwaka 2020/21 Wilaya imezalisha Tani **112,685** za wanga na nafaka na tani **12,855** za jamii ya mikunde. Aidha wilaya ina ziada ya tani **55,999.5** za (wanga na nafaka) na tani **2,169.4** za jamii ya mikunde.

##### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ina wakulima wa korosho **25,042** wenye jumla ya mikorosho **3,338,530** kwa kipindi cha miaka **2** wakulima wamezalisha korosho tani **21,057,726** mwaka 2019/20, na tani **21,992,353** kwa mwaka 2020/21 kwa sasa wakulima wanaendelea na upulizaji wa mikorosho na wanaishukuru serikali ya awamu ya **6** kwa kupanga na kuwapa pembejeo za mikorosho tani **2,402** za salfa ya unga, lita **23567** ubwirunga, lita **21,346** za Blaiti na lita **15,416** za wadudu bure katika musimu wa 2021/22. Ambapo hadi Agosti 30, 2021 Wakulima tumepokea **57.9%** za salfa ya unga, **82.6%** Ubwiriunga, **66.3%** ya Blaiti na **91.5%** ya wadudu.

#### **5.0 VIWANDA**

##### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ina viwanda **4** vya kati, kati ya hivyo **3** vinafanyakazi na **1** hakifanyi kazi ina viwanda vidogo vidogo **103** vilivyo ajiri zaidi ya watu **229**. Wilaya imefanikiwa kuongeza Viwanda 2 vya kati vilivyojengwa na wazawa. Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuweka mazingira wezeshi ya ujenzi wa viwanda. Lengo la viwanda hivi ni kutengeneza ajira, soko na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima ya korosho, Alizeti na mahindi.

#### **6.0 BARABARA**

##### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya ina mtandao wa barabara wenye urefu wa **1,447.06** KM, kati ya hizo **86** KM ni za TANROAD na **1,361.06** km ni za TARURA. Aidha Wilaya ina **12.12** KM za lami kwa barabara zilizo chini ya TARURA. Wilaya ina ishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuendelea kutenga na kuleta fedha za ujenzi na ukarabati wa barabara zetu kwa kiwango cha changarawe na Lami. Ambapo kwa mwaka 2021/22 Wilaya imetengewa Bilioni **2** Kujenga kilometa **4** za barabara za Lami.

## **7.0 MAKUSANYO YA MADUHILI YA SERIKALI NA UWEZESHAJI WA VIJANA, WATU WENYE ULEMAVU NA WANAWAKE;**

### **Mheshimiwa Rais,**

Wilaya imekusanya **49.14%** ya makisio ya Tsh **1,682,780,000/=** ya **TRA**, **128.57%** ya makisio ya Tsh **70,000,000/=** ya kodi ya pango la Ardhi na **83%** makisio ya Tsh. **4,543,792,000/=** ya mapato ya Halmashauri kwa Mwaka wa fedha 2020/2021. Mafanikio haya yamechangiwa na matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA. Aidha Wilaya imetoa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali **78** kati yao vikundi vya vijana ni **25** Wanawake **46** na watu wenye ulemavu **7** kwa mwaka 2020/21. Wilaya inaendelea kuwezesha vijana, walemavu na wanawake kupata mikopo yenye masharti nafuu ambapo kwa mwaka 2021/2022 Wilaya imetenga jumla ya Tsh. **234,166,200/-** ikiwa ni **10%** ya mapato halisi Tsh. **2,341,662,000/-** ya bajeti idhinishwa

## **8.0 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI WAKATI WA MBIO MAALUM MWENGE WA UHURU MWAKA 2019.**

### **Mheshimiwa Rais.**

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2019 zilipitia miradi **14** ya sekta za Elimu, Afya Miundombinu, maji, Maendeleo ya Jamii, Utawala bora. Kati ya hiyo miradi **3** iliwekewa mawe ya msingi, miradi **9** ilikaguliwa na kuonwa. Miradi yote ilikuwa na thamani ya shilingi **1,981,747,555/=**. Kwa sasa miradi yote iliyowekewa mawe ya msingi imekamilika na inatumika.

## **9.0 MIRADI YA MAENDELEO YA WANANCHI WAKATI WA MBIO MAALUM ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021.**

### **Mheshimiwa Rais.**

Mbio maalum za Mwenge wa Uhuru mwaka **2021** zimepitia miradi **7** ya sekta za Elimu, Afya Miundombinu, maji, Viwanda, Maendeleo ya Jamii na utekelezaji wa ujumbe wa mwenge wa Uhuru. Kati ya hiyo **1** umefunguliwa, miradi **3** imezinduliwa, mradi **1** umewekewa jiwe la msingi, miradi **2** imeonwa na kukaguliwa miradi ya vijana na ujumbe wa mwenge. Miradi yote ina thamani ya Tsh. **1,722,812,765.74** kati ya hizo Tsh. **113,007,000/=** ni mchango wa jamii, Tsh. **48,000,000/=** ni mchango wa Halmashauri, Tsh **1,404,451,502.35** ni mchango wa serikali kuu na wahisani shilingi **157,354,263.39/=**.

## **10.0 MICHANGO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2021**

### **Mheshimiwa Rais,**

Makusanyo ya michango ya Mwenge wa Uhuru ndani ya Wilaya ya Newala ni Jumla ya **Tsh 16,800,00/=** kiasi kilichopatikana kutokana na mwitikio mzuri kwa wananchi wenye uzalendo na matumaini ili kutekeleza shughuli za Mwenge wa Uhuru. Aidha kiasi cha Tsh **1,576,000/=** kati fedha zilizochangwa na wananchi zimetumika kutekeleza mradi uliyopitiwa na Mwenge wa Uhuru mwaka 2021, na kiasi cha **Tsh 15,224,000/=** kimetumika katika maandalizi ya mapokezi na sherehe za mkasha wa Mwenge wa Uhuru

## **11.0 HITIMISHO**

### **Mheshimiwa Rais,**

Sisi wananchi wa Wilaya ya Newala tumepokea Mwenge wa Uhuru na tumeukimbiza **Km 81** ili ulete tumaini Upendo na heshima. Tunakupongeza kwa jitihada unazozifanya katika kusimamia matumizi sahihi ya mfumo wa TEHAMA, Lishe bora, kupambana na magonjwa ya kuambukiza VVU/UKIMWI na U-Viko (COVID-19), tunaungana nawe katika kuhamasisha wananchi kupitia kauli mbiu ya ujumbe wa Mwenge unaosema: **"TEHAMA NI MSINGI WA TAIFA ENDELEU; ITUMIKE KWA USAHIHI NA UWAJIBIKAJI"**. Pia tunakuahidi kuwa, Tutaulinda Mwenge wa Uhuru na kuukabidhi kwa wenzetu Wilaya ya Masasi ukiwa salama. Kwa niaba ya wananchi wa Newala tunawaomba wakimbiza Mwenge Kitaifa kheri na mafanikio katika safari yao ndefu hadi waufikishe salama Mwenge wa Uhuru siku ya kilele Mkoani Geita.

**Mungu Ibariki Afrika**

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Kazi iendelee**

.....  
Mwangi Rajab. Kundyia  
**MKUU WA WILAYA**  
**NEWALA**

**Kiambata: A1 – ORODHA WANKIKUNDI WANAOKABIDHIWA PIKIPIKI**

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA  
MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU 2021**

**ORODHA WANKIKUNDI WANAOKABIDHIWA PIKIPIKI KWENYE MWENGE WA UHURU MWAKA 2021**

<b>Na</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>AINA YA PIKIPIKI</b>	<b>GHARAMA YA PIKIPIKI</b>	<b>GHARAMA YA USAJILI, KUFUNGA NA BIMA</b>	<b>JUMLA KUU</b>
1	JUSTINE MICHAEL MCHANYAMBI	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
2	SHEPHA STAMILI MOHAMEDI	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
3	EMANUEL LENATUS NICHOLUS	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
4	JACKSON EZEKIEL MTANDA	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
5	LEONARD FULGANCE NAMBUNGA	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
6	JABIRI SALUM ISMAIL	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
7	ASHIRAFU SAIDI LIKWANDA	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
8	ALLY MUSSA ALLY	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
9	SELEMANI FRANCIS VINTAN	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
10	FARAJI HAKIKA HAMISI	SINORAY	2,200,000	130,000	2,330,000
<b>JUMLA KUU</b>			<b>22,000,000</b>	<b>1,300,000</b>	<b>23,300,000</b>

**Kiambata: A2 – ORODHA WANKIKUNDI WANAOKABIDHIWA PIKIPIKI**

**HALMASHAURI YA WILAYA NEWALA  
MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU 2021**

**ORODHA WANKIKUNDI WANAOKABIDHIWA PIKIPIKI KWENYE MWENGE WA UHURU MWAKA 2021**

<b>Na</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>AINA YA PIKIPIKI</b>	<b>GHARAMA YA PIKIPIKI</b>	<b>GHARAMA YA USAJILI, KUFU NGA NA BIMA</b>	<b>GHARA ZA UENDESHAJI</b>	<b>JUMLA KUU</b>
1	HAMISI JUMA DADI	SINORAY	2,230,000/=	130,000/=	40,000/=	2,400,000/=
2	SHAZIRI ARABI MPUNGA	SINORAY	2,230,000/=	130,000/=	40,000/=	2,400,000/=
3	RAMADHANI SAIDI CHIPILA	SINORAY	2,230,000/=	130,000/=	40,000/=	2,400,000/=
4	SHABANI ISMAILI SANANE	SINORAY	2,230,000/=	130,000/=	40,000/=	2,400,000/=
5	MANZI SWALEHE NAMJUPA	SINORAY	2,230,000/=	130,000/=	40,000/=	2,400,000/=
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>11,150,000/=</b>	<b>650,000/=</b>	<b>200,000/=</b>	<b>12,000,000/=</b>
	KIKUNDI CHA TUNaweza	<b>TVS</b>	<b>8,400,000/=</b>	<b>250,000/=</b>	<b>50,000/=</b>	<b>8,700,000/=</b>
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>19,550,000/=</b>	<b>900,000/=</b>	<b>250,000/=</b>	<b>20,700,000/=</b>

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA**  
**GHARAMA ZA MIRADI YA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2019**

NA	SEKTA	MRADI	TUKIO	IDA DI	MCHANGANUO WA GHARAMA TSHS				
					WANANCHI	HALMASHA URI	S/KUU	WAHISANI	JUMLA
1	Utawala bora	Klabu ya kupinga rushwa	Kuona na kukagua maendeleo ya Klabu ya kupinga Rushwa shule ya sekondari Mnyambe	1	-	-	500,000	-	500,000
2	Afya	Utoaji wa huduma za Afya	Kuona na kukagua utoaji wa huduma za Afya	1	121,000,000	29,000,000		310,230,054	460,230,054
3	Elimu	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na bweni Mnyambe Sekondari	Kuweka jive la msingi	1	5,350,765	3,645,000	115,000,000	-	123,995,765
4	Utawala bora	Elimu ya uchaguzi	Kuzindua klabu ya kutoa elimu ya uchaguzi kijiji cha Mnyambe	1	-	500,000	3,000,000	-	3,500,000
5	Maendeleo ya Jamii	Shughuli za wanawake na vijana wajasiriamali	Kuona na kukagua shughuli za ujasiriamali	1	-	32,000,000	-	-	32,000,000
6	Maji	Uhifadhi wa chanzo cha maji Mitema	Kuona , kukagua na kupanda miti chanzo cha maji, ukarabati wa visima virefu sita (06) na kushiriki zoezi la upandaji wa miti	1	-	800,000	584,597,736		585,397,736
7	Ujumbe wa mwenge wa uhuru 2019	Kuona na kupata taarifa ya Halmashauri katika juhudi ya Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rushwa, Malaria, UKIMWI na Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	Kuona na kupata taarifa ya Halmashauri katika juhudi ya Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rushwa, Malaria, UKIMWI na Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	1	-	3,000,000	2,000,000	-	5,000,000
	<b>JUMLA KUU</b>			<b>7</b>	<b>126,350,765</b>	<b>68,945,000</b>	<b>885,097,736</b>	<b>310,230,054</b>	<b>1,390,623,555</b>

## HALMASHAURI YA MJI NEWALA

## GHARAMA ZA MIRADI YA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2019

N A	SEKTA	MRADI	TUKIO	IDA DI	MCHANGANUO WA GHARAMA TSHS				
					WANANCHI	HALMA	S/KUU	WAHISANI	JUMLA
1	Utawala bora	Klabu ya kupinga rushwa	Kuona na kukagua maendeleo ya Klabu ya kupinga Rushwa shule ya sekondari Mtangalanga	1	-	-	-	-	-
2	AFYA	Ujenzi wa zahanati ya Mtaa wa Tupendane	Kuweka jiwe la msingi na kupanda miti.	1	13,735,000	17,195,000	-	101,162,500	132,092,500
3	Elimu	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, ofisi, matundu 6 ya vyoo katika shule ya sekondari Newala	Kufungua vyumba vya madarasa	1	1,800,000		46,600,000	-	48,400,000
4	Miundombinu	Mradi wa matengenezo wa barabara ya Elimu kiwango cha lami.	Kuweka jiwe la msingi kipande cha km 1	1	-	-	356,432,000	-	356,432,000
5	Maendeleo ya Jamii	Shughuli za wanawake na vijana wajasiriamali	Kuona na kukagua shughuli za ujasiriamali	1	-	54,000,000	-	-	54,000,000
6	Maji	Uhifadhi wa chanzo cha maji Mkunya	Kuona , kukagua na kupanda miti	1	-	200,000			200,000
7	Ujumbe wa mwenge wa uhuru 2019	Kuona na kupata taarifa ya Halmashauri katika juhudi ya Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rushwa, Malaria, UKIMWI na Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	Kuona na kupata taarifa ya Halmashauri katika juhudi ya Mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Rushwa, Malaria, UKIMWI na Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa	1	-	-	-	-	-
	<b>JUMLA KUU</b>			<b>7</b>	<b>15,535,000</b>	<b>71,395,000</b>	<b>403,032,000</b>	<b>101,162,500</b>	<b>591,124,500</b>

**Kiambata: C1 HALI YA UTEKELEZAJI MIRADI YA MWENGE 2019**

**TAARIFA YA UENDELEU WA MIRADI ILIYOZINDULIWA/KUWEKEWA MAWE YA MSINGI NA VIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE  
WA UHURU 2019 – HALMASHAURI YA MJI**

Na	Jina la mradi	Hatua wakati wa mbio za Mwenge			Hali halisi ya sasa ya mradi
		kuzinduliwa	Jiwe la Msingi	Kukaguliwa	
Mwaka 2019					
1	Klabu ya kupinga rushwa			√	Klabu ya inaendelea baada ya kufunguliwa
2	Ujenzi wa zahanati ya Mtaa wa Tupendane		√		Mradi umekamilika na zahanati inatoahuduma
3	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa, ofisi, matundu 6 ya vyoo katika shule ya sekondari Newala	√			Madarasa na ofisi zinatumiwa
4	Mradi wa matengenezo wa barabara ya Elimu kiwango cha lami.		√		Mradi umekamilikaa na unatumika
5	Shughuli za wanawake na vijana wajasiriamali			√	Vinaja na wanawake wajasiriamali wanaendelea na shughuli zao, urejeshaji wa mikopo unafanyika kwa mujibu wa mikataba
6	Uhifadhi wa chanzo cha maji Mkunya			√	Hifadhi inaendelea kutoa huduma ya maji

**Kiambata: C2 – HALI YA UTEKELEZAJI MIRADI YA MWENGE 2019**

**TAARIFA YA UENDELEU WA MIRADI ILIYOZINDULIWA/KUWEKEWA MAWE YA MSINGI NA VIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE  
WA UHURU 2019- HALAMASHAURI YA WILAYA**

Na	Jina la mradi	Hatua wakati wa mbio za Mwenge			Hali halisi ya sasa ya mradi
		Kuzinduliwa	Jiwe la Msingi	Kukaguliwa	
Mwaka 2019					
1	Klabu ya kupinga rushwa			√	Klabu ya wapinga rushwa inaendelea baada ya kufunguliwa
2	Utoaji wa huduma za Afya			√	Huduma zinaendelea kutolewa
3	Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa na bweni Mnyambe Sekondari		√		Madarasa na bweni yanatumika
4	Elimu ya uchaguzi	√			Kikundi bado kinatumika katika utoaji wa elimu katika chaguzi za marudio
5	Shughuli za wanawake na vijana wajasiriamali			√	Vijana na wanawake wajasiriamali wanaendelea na shughuli zao, urejeshaji wa mikopo unafanyika kwa mujibu wa mikataba
6	Uhifadhi wa chanzo cha maji Mitema			√	Hifadhi inaendelea kutoa huduma ya maji

**HALI YA MIRADI ILIYOWEKEWA MAWE YA MSINGI NA VIONGOZI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2019**



***HALI YA MRADI WA ZAHANATI MWAKA 2019***



***HALI YA SASA YA ZAHANATI MWAKA 2021***



***MRADI WA BARABARA YA ELIMU MWAKA 2019***



***BARABARA YA ELIMU INATUMIKA***

**Kiambata: E –UTEKELEZAJI WA MAAGIZO YA MWENGE 2019**

**MAAGIZO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2019**

<b>Na.</b>	<b>Mradi</b>	<b>Agizo</b>	<b>Utekelezaji</b>
1.	Ujenzi wa zahanati ya Mtaa wa Tupendane	Mabomba ya kupitishia maji taka yabadilishwe kutoka Class A na kuwekwa Class C.	Agizo limezingatiwa na mabomba hayo yamebadilishwa.

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA  
MIKOPO YA WANAWAKE NA VIJANA 2019**

**ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA VILIVYOKOPESHA WAKATI WA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2019 NA HALI YA  
MAREJESHO**

NA	JINA LA KIKUNDI	KATA	MKOPO TOLEWA	SHUGHULI	MAREJESHO	DENI	AINA YA KIKUNDI
1	UKOMBOZI	MAKONGA	3,000,000	VICOBA NA KILIMO	3,000,000	-	WANAWAKE
2	MACHIMBO	LUCHINGU	2,000,000	UBANGUAJI KOROSHO	2,000,000	-	WANAWAKE
3	JIAMINI	LUCHINGU	4,000,000	UUZAJI MCHELE	3,604,000	396,000	WANAWAKE
4	MAENDELEO	MTUMACHI	4,000,000	UBANGUAJI KOROSHO	4,000,000	-	WANAWAKE
5	JITUME	MKUNYA	3,000,000	KILIMO CHA UYOGA	3,000,000		WANAWAKE
6	MSHIKAMANO	LUCHINGU	3,000,000	USHONAJI	2,950,000	50,000	WANAWAKE
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>19,000,000</b>		<b>18,554,000</b>	<b>446,000</b>	
7	JIAMINI	NANGWALA	4,000,000	USHONAJI	2,630,000	1,370,000	VIJANA
8	MAJENGO MARKET	MAKONGA	3,000,000	UUZAJI VIFAA VYA UJENZI	2,898,000	102,000	VIJANA
9	MUUNGANO	KILIDU	2,500,000	UFUGAJI	2,500,000	-	VIJANA
10	UPENDANO	NANGWALA	2,000,000	USHONAJI	2,000,000	-	VIJANA
11	DUMANA	TULINDANE	3,000,000	UBANGUAJI KOROSHO	1,102,000	1,898,000	VIJANA
12	MAYONET	MAKONGA	3,500,000	KILIMO NA UFUGAJI	3,175,000	325,000	VIJANA
13	AGRIBUSSNESS	MTONYA	3,000,000	KILIMO BUSTANI	2,518,900	481,100	VIJANA
14	AMANI	NANGWALA	2,500,000	UTENGENEZAJI SABUNI ZA MICHE	1,895,000	605,000	VIJANA
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>23,500,000</b>		<b>18,718,900</b>	<b>4,781,100</b>	
15	JIKOMBOE	JULIA	2,500,000	UFUGAJI KUKU	1,374,000	1,126,000	WALEMAVU
16	TUUNGANE	MNEKACHI	3,500,000	UBANGUAJI KOROSHO	3,500,000		WALEMAVU
17	LIUTE(WALEMAVU)	NAMIYONGA	2,000,000	UBANGUAJI KOROSHO	1,050,000	950,000	WALEMAVU
18	USHIRIKA	JULIA	3,500,000	SABUNI,VIKAPU NA BATIKI	3,360,000	140,000	WALEMAVU
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>11,500,000</b>		<b>9,284,000</b>	<b>2,216,000</b>	
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>54,000,000</b>		<b>46,556,900</b>	<b>7,443,100</b>	

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA**  
**MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 -JUNI 2021**  
**ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU VILIVYOKOPESHWA KWA FEDHA ZA 10%**

	JINA LA KIKUNDI	KATA	IDADI YA WANUFAIKA	MKOPO TOLEWA	SHUGHULI	MAREJESHO	BAKI	AINA YAKIKUNDI
1	USHIRIKA POSTA	NANGWALA	10	10,000,000	USUSI NA SALUNI	1,650,000	8,350,000	WANAWAKE
2	HIARY	LUCHINGU	10	4,000,000	MAMA LISHE	0	4,000,000	WANAWAKE
3	JITAMBUE	LUCHINGU	10	2,000,000	UTENGENEZAJI MAKAPU NA USHONAJI	0	2,000,000	WANAWAKE
4	NASA	MTONYA	10	8,000,000	USINDIKAJI VYAKULA	2,350,000	5,650,000	WANAWAKE
5	MASALO	MTONYA	10	5,000,000	UUZAJI WA NYANYA	1,150,000	3,850,000	WANAWAKE
6	ZAIDI	LUCHINGU	10	3,000,000	UUZAJI SAMAKI NA UTENGENEZAJI MIKOBA	270,000	2,730,000	WANAWAKE
7	MSHIKAMANO VIKOBA	MTUMACHI	10	3,000,000	UTENGENEZAJI SABUNI NA UBANGUAJI KOROSHO	300,000	2,700,000	WANAWAKE
8	MAKUBALIANO	NANGWALA	10	2,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	550,000	1,450,000	WANAWAKE
9	TUNAWEZA	NANGWALA	10	2,000,000	USHONAJI	590,000	1,410,000	WANAWAKE
10	MKIMANGA	NANGWALA	10	3,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	550,000	2,450,000	WANAWAKE
11	TUINUANE	NANGURUWE	10	1,500,000	UFUGAJI KUKU	450,000	1,050,000	WANAWAKE
12	TEGEMEO	LUCHINGU	10	2,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	430,000	1,570,000	WANAWAKE
13	TUVAMO	NANGWALA	10	2,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	200,000	1,800,000	WANAWAKE
14	KUDRA	NANGWALA	10	2,500,000	UTENGENEZAJI WA SABUNI NA MAKAPU	1,000,000	1,500,000	WANAWAKE
15	TEGEMEO	MAHUMBIKA	10	2,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	600,000	1,400,000	WANAWAKE
16	USTAWI	MCHOLI II	10	5,000,000	UBANGUAJI WA KOROSHO	0	5,000,000	WANAWAKE
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>160</b>	<b>57,000,000</b>		<b>10,090,000</b>	<b>46,910,000</b>	
1	NACHITULO	LUCHINGU	10	2,024,000	BABA LISHE	600,000	1,424,000	VIJANA
2	MPAKANI	MCHOLI I	10	5,000,000	KILIMO CHA BUSTANI	200,000	4,800,000	VIJANA
3	MSHIKAMANO	NANGWALA	10	3,000,000	UUZAJI WA NYANYA	410,000	2,590,000	VIJANA

4	KECHI WELDERS	NANGWALA	10	3,000,000	UCHOMELEAJI	0	3,000,000	VIJANA
5	NGUVU KAZI	MCHOLI I	10	2,500,000	KILIMO CHA BUSTANI	0	2,500,000	VIJANA
6	TUTAPAMBANA	MTONYA	10	2,500,000	USHONAJI	530,000	1,970,000	VIJANA
7	PAMOJA TUNAWWEZA	MKULUNG'ULU	10	3,000,000	KILIMO CHA BUSTANI	210,000	2,790,000	VIJANA
8	TUNAWWEZA	MCHOLI I	10	4,000,000	KILIMO CHA BUSTANI	200,000	3,800,000	VIJANA
9	BODA BODA NA 3	NANGWALA	10	23,590,000	UENDESHAJI WA BODABODA	0	23,590,000	VIJANA
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>90</b>	<b>48,614,000</b>		<b>2,150,000</b>	<b>46,464,000</b>	
1	WALEMAVU TUNAWWEZA	JULIA	8	500,000	UFUGAJI KUKU	0	500,000	WALEMAVU
2	JUHUDI WALEMAVU	MAKONGA	5	500,000	UZAJI MAYAI	50,000	450,000	WALEMAVU
3	NJIA NNE	NANGWALA	5	500,000	UBANGUAJI KOROSHO	51,000	449,000	WALEMAVU
4	TUUNGANE	MNEKACHI	10	3,000,000	UBANGUAJI KOROSHO	600,000	2,400,000	WALEMAVU
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>28</b>	<b>4,500,000</b>		<b>701,000</b>	<b>3,799,000</b>	
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>278</b>	<b>110,114,000</b>		<b>12,941,000</b>	<b>97,173,000</b>	

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA**  
**MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU KWA KIPINDI CHA JULAI 2020 -JUNI 2021**  
**ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU VILIVYOKOPESHWA KWA FEDHA ZA 10%**

NO	JINA KA KIKUNDI	IDADI YA WANAKIKUNDI	KATA	SHUGHULI	KIASI CHA MKOPO	RIBA	MAREJESHO	BAKI	AINA YA KIKUNDI
1	WELDING CAMP	10	KITANGARI	WELDING(KUCHOMEA)	3,000,000.00			3,000,000.00	VIJANA
2	BODABODA	10	KITANGARI	BODABODA	22,500,000.00		2,850,000.00	20,250,000.00	VIJANA
3	TUUNGANE	5	MAKUKWE	UBANGUAJI KOROSHO	4,000,000.00			4,000,000.00	VIJANA
4	CHILANGALA WORKSHOP	10	CHILANGALA	USEREMALA/UWASHI	5,600,000.00			5,600,000.00	VIJANA
5	BODABODA VIJANA	5	MKWEDU	BODABODA(USAFIRISHAJI)	3,450,000.00				VIJANA
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>40</b>			<b>38,550,000.00</b>		<b>2,850,000.00</b>	<b>32,850,000.00</b>	
6	MAELEWANO	10	KITANGARI	UTENGENEZAJI WA SABUNI	4,000,000.00			4,000,000.00	WANAWAKE
7	MNUNGA	10	KITANGARI	BIASHARA NDOGONDOGO	3,500,000.00			3,500,000.00	WANAWAKE
8	TUKI	9	MUUNGANO	UFUGAJI WA KUKU	3,000,000.00			3,000,000.00	WANAWAKE
9	G -SEVEN	7	MCHEMO	BIASHARA NDOGONDOGO/UFUGAJI WA KUKU	3,000,000.00		204,000.00	3,000,000.00	WANAWAKE
10	MAPAMBANO	10	KITANGARI	BIASHARA YA SAMAKI	4,000,000.00			4,000,000.00	WANAWAKE
11	UPENDO A	10	MAPUTI	UBANGUAJI KOROSHO	6,000,000.00			6,000,000.00	WANAWAKE
12	TUPWEHELANE	14	NANDWAHI	UFUMAJI NA UTENGENEZAJI WA SABUNI	3,000,000.00			3,000,000.00	WANAWAKE
13	UMOJA NI NGUVU	12	NAKAHAKO	KILIMO /UFUGAJI	4,000,000.00			4,000,000.00	WANAWAKE
14	GANGA NJAA	11	MNYEU	BIASHARA NDOGONDOGO	2,797,000.00			2,797,000.00	WANAWAKE

	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>93</b>			<b>33,297,000.00</b>		<b>204,000.00</b>	<b>33,297,000.00</b>	
15	TUNAWEZA	3	MAPUTI	BAJAJI(USAFIRISHAJI)	7,500,000.00			7,500,000.00	WALEMAVU
16	TUJALIANE	5	MNYEU	UFUGAJI WA KUKU/BIASHARA YA NYAMA	3,200,000.00			3,200,000.00	WALEMAVU
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>8</b>			<b>10,700,000.00</b>			<b>10,700,000.00</b>	
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>141</b>			<b>82,547,000.00</b>		<b>3,054,000.00</b>	<b>76,847,000.00</b>	

**Kiambata: H1 - MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU  
KUPITIA FEDHA ZA 10% MWAKA 2019/2020**

**HALMASHAURI YA MJI NEWALA  
MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU KWA MWAKA 2019/2020  
ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU VILIVYOKOPESHWA NA HALI YA MAREJESHO**

1	JINA LA KIKUNDI	AINA YA KIKUNDI	IDADI YA WANUFAIKA			SHUGHULI	MKOPO TOLEWA	MAREJESHO	BAKI
			2	3	5				
1	UVUMILIVU	VIJANA	2	3	5	Ufugaji samaki na kilimo cha Bustani	5,000,000	860,000.00	4,140,000
2	TUNAWEZA	VIJANA	0	5	5	Kilimo cha Bustani	3,000,000	,000,000.00	-
3	ONJACHI	VIJANA	2	3	5	Kilimo cha Ndizi	3,000,000	2,100,000.00	900,000
4	WASAMBAZAJI WA SAMAKI	VIJANA	2	3	5	Uuzaji wa Samaki	3,000,000	2,840,000.00	160,000
5	NANGWALA STARS	VIJANA	0	6	6	Ushonaji	1,000,000	650,000.00	350,000
6	WAMANTA	VIJANA	0	5	5	Baba Lishe	2,000,000	1,800,000.00	200,000
7	MPAKANI	VIJANA	0	5	5	Kilimo cha Bustani	5,000,000	5,000,000.00	-
8	TUIMARIKE	VIJANA	2	8	10	Ufugaji wa kuku	3,000,000	2,140,000.00	860,000
9	KISUNA	VIJANA	2	3	5	Utengenezaji (culture)	1,000,000	915,000.00	85,000
10	UKOMBOZI	VIJANA	5	7	12	Ubanguaji korosho	3,500,000	1,417,000.00	2,083,000
11	UJENZI	VIJANA	0	5	5	Useremala	2,500,000	600,000.00	1,900,000
12	SOUTHERN GRP	VIJANA	2	4	6	Ufugaji kuku na Welding	3,000,000	1,200,000.00	1,800,000
13	TAILORING	VIJANA	3	7	10	Ushonaji	2,000,000	230,000.00	1,770,000
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>20</b>	<b>64</b>	<b>84</b>		<b>37,000,000</b>	<b>22,752,000</b>	<b>14,248,000</b>
14	TANO BORA	WANAWAKE	5	0	5	Utengenezaji batiki	1,000,000	500,000.00	500,000
15	JUHUDI	WANAWAKE	5	0	5	Mama Lishe	3,500,000	2,990,000.00	510,000
16	NEWALA GROUP OF TALENT	WANAWAKE	5	0	5	Utengenezaji Viatu na Mikoba	4,000,000	3,750,000.00	250,000
17	UHURU	WANAWAKE	5	0	5	Ubanguaji korosho	2,500,000	2,402,000.00	98,000
18	TUPENDANE	WANAWAKE	5	0	5	Uuzaji samaki	2,500,000	1,175,000.00	1,325,000

19	WAHIVI HIVI	WANAWAKE	7	0	7	Ubanguaji Korosho	4,000,000	4,000,000.00	-
20	KIANGAZA	WANAWAKE	11	0	11	Ubanguaji korosho	3,500,000	1,905,000.00	1,595,000
21	TUMEJIKUBALI	WANAWAKE	6	0	6	Mama Lishe	3,500,000	3,500,000.00	-
22	TUMAINI	WANAWAKE	8	0	8	Utengenezaji batiki	3,000,000	590,000.00	2,410,000
23	USTAWI	WANAWAKE	10	0	10	Ubanguaji korosho	1,000,000	1,000,000.00	-
24	MATOKEO	WANAWAKE	12	0	12	Ubanguaji korosho	3,500,000	1,500,000.00	2,000,000
25	TUPENDANE	WANAWAKE	5	0	5	Mama Lishe	3,000,000	2,500,000.00	500,000
26	BRIGHT FUTURE	WANAWAKE	5	0	5	Ubanguaji korosho	3,000,000	980,000.00	2,020,000
27	TULINGE	WANAWAKE	8	0	8	Ubanguaji korosho	2,000,000	510,000.00	1,490,000
28	TUVALOLE	WANAWAKE	8	0	8	Utengenezaji sabuni na Batiki	2,000,000	1,460,000.00	540,000
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>105</b>	<b>0</b>	<b>105</b>		<b>42,000,000</b>	<b>28,762,000</b>	<b>13,238,000</b>
29	UPENDO	WALEMAVU	0	5	5	Ubanguaji korosho	2,000,000	565,000.00	1,435,000
30	PAMBANA	WALEMAVU	0	5	5	Ushonaji	2,000,000	1,470,000.00	530,000
31	TEGEMEZI	WALEMAVU	0	5	5	Ufugaji kuku	2,000,000	1,200,000.00	800,000
32	TUJITUME	WALEMAVU	1	4	5	Useremala	2,000,000	1,220,000.00	780,000
33	THE ONE	WALEMAVU	0	5	5	Utengenezaji Batiki na sabuni	2,000,000	2,000,000.00	
34	HEKIMA	WALEMAVU	1	6	7	Useremala na Ushonaji	2,500,000	1,593,000.00	907,000
35	FARAJA	WALEMAVU	6	0	6	Utengenezaji sabuni za Maji	2,500,000	450,000.00	2,050,000
	<b>JUMLA NDOGO</b>		<b>8</b>	<b>30</b>	<b>38</b>		<b>15,000,000</b>	<b>8,498,000</b>	<b>6,502,000</b>
	<b>JUMLA KUU</b>		<b>133</b>	<b>94</b>	<b>227</b>		<b>94,000,000</b>	<b>60,012,000</b>	<b>33,988,000</b>

**Kiambata: H2 - MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU  
KUPITIA FEDHA ZA 10% MWAKA 2019/2020**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA  
MIKOPO YA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU KWA MWAKA 2019/2020  
ORODHA YA VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WALEMAVU VILIVYOKOPESHWA NA HALI YA MAREJESHU**

NO	JINA LA KIKUNDI	IDADI YA WANUFAIKA	KATA	SHUGHULI	MKOPO TOLEWA	MAREJESHO	BAKI	AINA YA KIKUNDI
1	UPENDO A	10	MAPUTI	UBANGUAJI KOROSHO	3,000,000.00	3,000,000.00	-	WANAWAKE
2	JIPE MOYO	6	MPWAPWA	UFUGAJI KUKU/BIASHARA NDOGONDOGO	2,000,000.00	2,000,000.00		WANAWAKE
3	MMAITECHI	5	MKWEDU	UBANGUAJI KOROSHO/UFUGAJI KUKU	4,000,000.00	-	4,000,000.00	WANAWAKE
4	MUUNGANO	14	MCHEMO	KILIMO CHA ALIZETI	3,000,000.00	3,000,000.00	-	WANAWAKE
5	TUVENE	10	CHITEKETE	UFUGAJI NYUKI	4,000,000.00	4,000,000.00	-	WANAWAKE
6	MPE RAHA	8	MDIMBA MPELE PELE	UFUGAJI KUKU	4,000,000.00	4,000,000.00	-	WANAWAKE
7	JIPE MOYO	10	CHITEKETE	USINDIKAJI MUHOGO	3,000,000.00	1,630,000.00	1,370,000.00	WANAWAKE
8	WAZO LETU	8	MUUNGANO	KILIMO CHA ALIZETI	3,000,000.00	982,000.00	2,018,000.00	WANAWAKE
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>63</b>			<b>26,000,000.00</b>	<b>18,612,000.00</b>	<b>7,388,000.00</b>	
9	MAENDELEO	10	CHIHANGU	UFUGAJI KUKU	2,500,000.00	1,770,000.00	730,000.00	VIJANA
10	LITIPU	6	KITANGARI	BIASHARA NDOGO NDOGO	5,000,000.00		5,000,000.00	VIJANA
11	TUVAMO	5	KITANGARI	UFUGAJI KUKU	4,000,000.00		4,000,000.00	VIJANA
12	UMMOJA WA WAFUGAJI KUKU	8	MAKUKWE	UFUGAJI KUKU	3,000,000.00	250,000.00	2,750,000.00	VIJANA
13	MAMA NTLIE	6	KITANGARI	MAMA NTLIE	3,000,000.00	140,000.00	2,860,000.00	VIJANA
14	SONGONI POULTRY FARM	6	KITANGARI	UFUGAJI KUKU	6,000,000.00		6,000,000.00	VIJANA
15	MAFANIKIO	8	KITANGARI	UFUGAJI KUKU	4,000,000.00	2,500,000.00	1,500,000.00	VIJANA
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>49</b>			<b>27,500,000.00</b>	<b>4,660,000.00</b>	<b>22,840,000.00</b>	
16	MAENDELEO	6	MAKUKWE	UFUGAJI KUKU/UBANGUAJI KOROSHO	3,000,000.00	1,000,000.00	2,000,000.00	WALEMAVU
	<b>JUMLA NDOGO</b>	<b>6</b>			<b>3,000,000.00</b>	<b>1,000,000.00</b>	<b>2,000,000.00</b>	
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>118</b>			<b>56,500,000.00</b>	<b>24,272,000.00</b>	<b>32,228,000.00</b>	

## **SALAMU ZA MKUU WA WILAYA YA NEWALA KWENYE**

### **MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU 31.08.2021**

Mhe. Claudia Kitta, Mkuu wa Wilaya Masasi,

Ndugu, Luteni Josephine Paul Mwambashi, Kiongozi wa Mbio maalum za mwenge Kitaifa 2021

Ndugu, Wakimbiza Mwenge wote Kitaifa na wakufunzi

Ndugu, Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama (M)

Ndugu, Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama (W)

Ndugu. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Newala

Ndugu. Katibu wa CCM Wilaya ya Newala

Wahe. Wabunge wa Majimbo ya Newala Mji na Newala vijijini

Wah. Madiwani

Ndugu. Viongozi Vyama vya Siasa

Ndugu. Viongozi wa Dini, Wakuu wa Taasisi na Mashirika na binafsi, Watendaji wa Serikali, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali, Wanahabari, Wananchi wote wa Newala mliahudhuria Mabibi na Mabwana

#### **Mhe. Mkuu wa Wilaya na Ndugu Kiongozi wa Mbio Maalum za Mwenge Kitaifa**

Napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwepo kwenye eneo la makabidhiano ya Mwenge wetu wa Uhuru hapa Kijiji cha Lidumbe Mtoni. Nawapongeza sana Wakimbiza Mwenge Kitaifa pamoja na wakufunzi wao kwa kuukimbiza Mwenge wa Uhuru salama na kueneza ujumbe wa Mwenge kwa wananchi wa Wilaya ya Newala.

#### **Mhe. Mkuu wa Wilaya na Ndugu Kiongozi wa Mbio Maalmu za Mwenge Kitaifa**

Mwenge wa Uhuru ukiwa Wilaya ya Newala umekimbizwa umbali wa km **81**, tarafa **2** kata **10** na vijiji **23**. Aidha, Mwenge wa Uhuru umetembelea miradi **7** ambapo ulifungua mradi **1**, ulizindua mradi **3**, uliweka jiwe la msingi miradi **1** na ulikagua na kuona miradi **2**. Miradi hii imezingatia ujumbe wa mwenge wa mwaka 2021 kwa ujumla Miradi yote **7** ina jumla ya thamani ya Tsh. **1,722,812,765.39** ambapo mchango wa Wananchi ni **6.56%**, Wilaya **2.79%**, Serikali Kuu **81.52%** na Wahisani **9.13%**. Aidha, wananchi wengi wa Newala wameuona na kuushangilia mwenge huu, na wamefuatilia matukio yote ya mwenge kupitia redio Newala iliyokua ikirusha matukio yote ya shughuli za mwenge hewani.

#### **Mhe. Mkuu wa Wilaya na Ndugu Kiongozi wa Mbio Maalum za Mwenge Kitaifa**

Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 umejionea juhudi za wananchi wa Newala katika kutunza vyanzo vya maji kwa kutambua, kuthamini jitihada zinazo fanywa na serikali ya awamu ya tano katika kulinda, kuhifadhi vyanzo na miundombinu ya maji na kuzingatia matumizi sahihi ya maji ili kuwa na maendeleo endelevu ya rasilimali maji. Aidha Mwenge wa Uhuru mwaka 2021 umepata taarifa

ya wananchi wa Newala wanavyotambua umuhimu wa kushiriki uchaguzi na kuchagua viongozi safi watakao shirikiana na Serikali ya awamu ya tano kuleta maendeleo wilayani Newala.

**Mhe. Mkuu wa Wilaya na Ndugu Kiongozi wa Mbio Maalum za Mwenge Kitaifa**

Mwenge wetu umejionea juhudi za wananchi wa Wilaya ya Newala katika mapambano dhidi ya maadui wa maendeleo ambao ni **UMUHIMU NA UZINGATIAJI WA LISHE BORA, RUSHWA, DAWA ZA KULEVYA, UKIMWI na MALARIA**. Aidha mwenge wa Uhuru mwaka 2021 umehamasisha na kuhimiza wananchi kupima na kujua afya zao pamoja na matumizi sahihi ya vyandarua. Vilevile umehimiza wananchi kuhudhuria vituo vya upimaji na ushauri nasaha kwa hiari, ufuasi wa dawa za ARV kwa wanaozitumia.

**Mhe. Mkuu wa Wilaya na Ndugu Kiongozi wa Mbio Maalum za Mwenge Kitaifa**

Sisi wananchi Wilaya ya Newala tunakukabidhi mwenge wa Uhuru ukiwa unang'aa, unameremeta, pamoja na wakimbiza mwenge **6** wa kitaifa, wakufunzi wao na wakimbiza mwenge **9** wa mkoa wakiwa salama.

NAWASILISHA

**MWENGE OYEEEEEE!!  
WILAYA YA NEWALA OYEEEE!!!**

.....  
**MHE. MWANGI RAJAB KUNDYA  
MKUU WA WILAYA YA NEWALA**

# ORODHA YA WAKIMBIZA MWENGE WA UHURU KITAIFA MWAKA 2021

